# Nipashe

Jumanne Julai 2, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579959

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Shahidi ataja damu kesi ya kina Mbowe

UKURASA 3




UKURASA 13

# Mfanyabiashara adaiwa kutekwa

• **Ni** msaidizi wa Zitto, bosi wake aweka mambo bayana kuhusu sakata zima... *Endelea ukurasa wa 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**VETA YABUNI KIBAO CHA KUFULIA NGUO KIURAHISI**

MAMLAKA ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (Veta), imetambulisha teknolojia mpya ya kibao cha kufulia nguo za aina...

**UKURASA WA 4**

**MAKALI YA KUNGUNI MAJUMBANI, SHULENI**

KATIKA toleo letu la jana tuliona jinsi wadudu aina ya kunguni wanavyosababisha usumbufu kwa taasisi hususan shule...

**UKURASA WA 26**

**WASOMI WACHAPISHA KAZI MAJARIDA FEKI**

RAIS wa Akademia ya Sayansi, Prof. Yunus Mgaya, amesema watafiti wengi nchini wameingia kwenye mkumbo wa...




Kijiko cha kampuni ya CCECC, kikitoa udongo kuwanasua tembo wawili waliokwama kwenye shimo lenye matope kwa siku mbili katika Pori Tengefu la Muhesi, Itigi, wilayani Manyoni, mkoa wa Singida mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MCHEKADONA**

## Wadaiwa sugu wa TBA sasa matatani

UKURASA 3

## Msekwa, Zitto wafunguka kuvuliwa ubunge wa Lissu

UK. 2


**MICHEZO** **SAMATTA AKATAA KUMFUATA ORIGI** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# Mfanyabiashara adaiwa kutekwa

**Enock Charles na Romana Mallya**

KIONGOZI Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, ameitaka serikali kuchukua hatua kuhusu kutoonekana kwa mfanyabiashara Raphael Ongangi, anayedaiwa kupotea kwa wiki moja sasa.

Jeshi la Polisi limekiri kupokea taarifa za madai ya kutekwa kwa mfanyabiashara huyo na linaendelea kuzifanyia kazi.

Akizungumza na vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana, Zitto alidai mfanyabiashara huyo ambaye ni raia wa Kenya, amekuwa nchini tangu mwaka 2002 na aliwahi kuwa msaidizi wake.

"Raphael alikuja hapa nchini tangu mwaka 2002 na alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kusomea shahada ya biashara, na akiwa nchini, alipata marafiki wengi wa Tanzania na hata kufunga ndoa na Mtanzania," alisema.

Zitto ambaye pia ni Mbunge wa Kigoma Mjini, alidai mfanyabiashara huyo alitekwa maeneo ya Osterbay jijini akiwa na mke wake, Veronica wakitokea shuleni kwa mtoto wao kulikokuwa na kikao cha wazazi.

Alidai kulitokea gari lililowazuia kwa mbele na waliokuwamo kuwatolea silaha aina ya bastola na kuwachukua wote wawili na baadaye mkewe aliachiwa, huku Raphael wakiondoka naye.

Zitto alidai tangu kutekwa kwa mfanyabiashara huyo Jumatatu Juni 24, mwaka huu, tayari ameshalifikisha suala hilo katika mamlaka mbalimbali za likiwamo Jeshi la Polisi alikoripoti kwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI).

Alidai ameripoti kwenye idara nyingi za serikali zinazohusu uchunguzi wa masuala nyeti na kutoa taarifa muhimu zikiwamo namba za magari yaliyotumika kumteka Raphael, lakini hawajafanikiwa kupata taarifa kutoka kwenye idara hizo kuhusu mfanyabiashara huyo.

Hata hivyo, Zitto alidai marafiki wa mfanyabiashara huyo wamefanikiwa kupata taarifa muhimu kuhusu magari yaliyotumika kumteka na alikowekwa mfanyabiashara huyo.

"Sisi marafiki wa Raphael kwa kutumia msaada wa marafiki zetu nje ya nchi, tumefanikiwa kupata alipowekwa Raphael baada ya kutekwa, pia tumefanikiwa kupata namba za magari yaliyomteka Raphael," Zitto alidai.

Kiongozi huyo wa ACT-Wazalendo aliiomba Serikali ya Kenya kufuatilia suala hilo, akiahidi kutoa ushirikiano kwayo kwa kuikabidhi taarifa walizofanikiwa kuzipata kuhusu mfanyabiashara huyo.

"Sisi tunaikabidhi Serikali ya Kenya ushahidi kwa kila mahali alipokuwa Raphael tangu siku ametekwa mpaka sasa," Zitto alisema.

INAENDELEA UK. 8



Kiongozi wa Chama cha ACT - Wazalendo, Zitto Kabwe, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kutekwa kwa aliyekuwa msaidizi wake, Raphael Ogangi, na kuiomba serikali kulichukulia uzito jambo hili ili kuweza kumpata kwa haraka. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Msekwa, Zitto wafunguka Lissu kuvuliwa ubunge

**Beatrice Shayo na Enock Charles**

SPIKA mstaafu Pius Msekwa na Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, wamefunguka kuhusu uamuzi uliofanywa na Spika Job Ndugai wa kumvua ubunge Tundu Lissu.

Ijumaa wakati wa kuahirisha mkutano wa Bunge la Bajeti, Spika Ndugai alitangaza kuwa Jimbo la Singida Mashariki liko wazi kutokana na Lissu kuwa mtoro bungeni na kutojaza fomu ya mali na madeni.

Akizungumzia uamuzi huo wa Spika Ndugai katika mahojiano na Nipashe jana, Msekwa alisema spika mwenzake huyo yuko sahihi kikatiba, akikumbusha kuwa hata kwenye uongozi wake aliwahi kuchukua uamuzi kama huo kwa kuwaondoa wabunge 50 kutokana na utoro.

Msekwa alisema mbunge yeyote anapaswa kumjulisha kwa maandishi na kuomba ruhusa ya kutohudhuria vikao vya Bunge na siyo Spika afuate yanayosemwa kwenye vyombo vya habari.

"Katiba inamtaka mbunge yeyote anayeshindwa kuhudhuria vikao vya Bunge kwa sababu yoyote, amjulishe Spika kwa maandishi ya barua na Spika atajibu barua hiyo, na kama hataridhika na barua hiyo, asihudhurie vikao, basi hatampa ruhusa ya kutohudhuria," Msekwa alisema na kuongeza:

"Haitoshi kusema kuwa magazeti yaliandika kwamba Lissu yuko hospitali, hiyo haitoshi, dhumuni la Katiba, Spika hawezi kutoa ruhusa kupitia magazeti, lazima mhusika mwenyewe aandike barua ya kuomba ruhusa," alisema.

Msekwa alisema kuwa kama Lissu hakufuata utaratibu huo, ndiyo sababu Spika akaamua kuchukua uamuzi huo.

"Hata mimi nilishawahi kuchukua uamuzi kama huo, nikawavua ubunge wabunge 50 wa Chama cha Wananchi (CUF). Chama chao kiliamua kususia vikao vya Bunge baada ya kushindwa uchaguzi.

"Wakatangaza katika magazeti kuwa wanasusia vikao vya bunge kwa hiyo wabunge wao hawatahudhuria vikao vya Bunge, walivyokosa vikao vitatu kama Katiba inavyotaka nikatangaza kuwavua

INAENDELEA UK. 8

# Majibu ya waziri madai fidia wakazi Kipunguni

**Na Beatrice Moses**

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, amesema suala la fidia za wakazi wa Kipunguni jijini Dar es Salaam wanaopaswa kuhama ili kupisha upanuzi wa uwanja wa ndege ni la kisheria.

Maelezo ya waziri huo yanatokana na swali aliloulizwa na gazeti hili jana kuhusu mkutano ulioandaliwa ili azungumze na wakazi wa Kipunguni Jumamosi, lakini hakufika ikidaiwa alipata dharura, hivyo kwenda bandarini.

Wakazi hao walicharuka mbele ya Mbunge wa Segerea, Bonna Kamoli, aliyeandaa mkutano huo, wakimjulisha kuwa wanamhitaji waziri huyo ili hawajulishe ni lini watalipwa fidia zao wanazodai kwa zaidi ya miaka 20.

"Suala unaloniulizia ni la kisheria, kama unahitaji ufafanuzi andika barua kwa Katibu wa Wizara," alisema Waziri Kamwele.

Mhandisi Kamwelwe ni Waziri wa Wizara hiyo tangu Julai 2018 ambapo mtangulizi wake ni Prof. Makame Mbarawa, aliyehamishiwa Wizara ya Maji.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kipunguni, Praxeda Mkandara, aliwatangazia wananchi hao kuahirishwa kwa mkutano huo hadi watakapoarifiwa tena.

Alieleza kuwa taarifa walizonazo ni kwamba waziri amepata dharura amekwenda Bandari ya Dar es Salaam kuna tishio la mgomo wa madereva.

Mwenyekiti huyo aliliambia gazeti hili kuwa tatizo hilo limekuwa ni kero kubwa kwa wananchi, limedumaza maendeleo yao huku baadhi ya wananchi wa Kipunguni Mashariki wakiamua kuendelea na ujenzi wa nyumba zao wakitarajia kufanyiwa tathmini.

"Ni kero kwa wananchi bora waambiwe ukweli maana jambo hili limeshughulikiwa na mawaziri karibu wanne, lakini hadi sasa hakuna suluhisho, mbunge wa upande wake amekuwa akijitahidi kukumbusha jambo hili lishughulikiwe," alisema.

Wakazi wa Kipunguni kwa nyakati tofauti wamekuwa wakilalamikia kucheleweshwa kwa ulipaji wa fidia hiyo, hatua ambayo imewafanya wengi washindwe kuyaendeleza maeneo hayo wakihofia kuhamishwa wakati wowote.

Mmoja wa wakazi hao, Hilda Kaijage, alisema ucheleweshwaji wa malipo ya fidia hiyo umewakwamisha kimaendeleo kwa kuwa imechukua miaka mingi bila kutolewa, pia wamekuwa wakiishi kama wapo kizuizini.

Mkazi mwingine, Mustafa Ahmed, anakumbuka wakati anajenga nyumba yake yenye vyumba sita saruji ilikuwa inauzwa shilingi 3,800 ikichangazwa na gharama za nauli ilikuwa 200 kwa mfuko mmoja.

Mbunge Kamoli alieleza kuwa jambo hilo la fidia limekuwa likimkosesha amani kwa kuwa anatambua ni haki ya wananchi hao kulipwa ili wajiendeleze kimaisha katika maeneo waliyopewa.

HABARI KITAIFA

# Veta yaja na kibao cha kufulia nguo kwa urahisi

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (Veta), imetambulisha teknolojia mpya ya kibao cha kufulia nguo za aina zote kwa urahisi na kwa haraka inayoonekana kuwavutia wananchi mbalimbali.

Teknolojia hiyo mpya iliyoletwa nchini na raia wa Japan, Ryuta Okamoto, inaelezwa kuwa itawakomboa wanawake wengi na watoto katika kazi za kufua nguo kwa kutumia mkono.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana wakati wa maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Biashara yaliyoanza rasmi Juni 28, mwaka huu, Okamoto ambaye ni Ofisa Maendeleo anayefanya kazi katika Wilaya ya Songea, mkoani Ruvuma kwa kujitolea kupitia Shirika la Maendeleo la Japan (JICA), alisema teknolojia hiyo ya kutumia kibao ilianzia Bara la Ulaya na kwenda nchini Japan, barani Asia.

Alisema alijifunza kutengeneza teknolojia hiyo kutoka kwa bibi yake na kwa sasa Wajapani wengi wanatumia, anaamini kuwa ujio wa teknolojia hiyo hapa nchini itawavutia Watanzania ambao wanaanza kuitumia na kuokoa muda mwingi wakati wa ufuaji.

Okamoto alisema teknolojia hiyo inamwezesha mtu kufua nguo moja kwa nusu dakika, hivyo kuokoa muda na kumrahisishia mtu kumaliza kazi ya kufua kwa haraka kisha kuendelea na shughuli zingine.

"Kibao hiki kinapatikana hapa Sabasaba kwa Sh. 5,000 na kazi ya kuvitengeneza inafanywa na wanafunzi wa Chuo cha Veta kutoka Songea wanaosomea kozi ya useremala, " alisema.




Rais John Magufuli akishuka kwenye ndege ya Shirika la Ndege la Tanzania, Air Tanzania (ATCL), baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Chato, mkoani Geita jana. Rais Magufuli amewasili katika Kijiji cha Mlimani, wilayani humo kwa mapumziko. **PICHA: IKULU**

# Shahidi ataja damu kesi ya Mbowe

**Na Hellen Mwango**

SHAHIDI wa tano, Inspekta Msaidizi Dk. Juma Alfani (54) katika kesi ya uchochezi inayomkabili Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe na wenzake, amedai mahakamani kwamba aliwapokea Koplo Rahim na Konstebo Fikiri wakiwa wanapiga kelele za kulalamika maumivu ya majeraha waliyopata kwenye maandamano.

Kadhalika, amedai kuwa Koplo Rahim alikuwa anaweweseka huku akilalamika maumivu shingoni kwa sababu alikuwa hajitambui na

INAENDELEA UK.8

# Wadaiwa sugu TBA matatani

**Na Christina Mwakangale**

WADAIWA sugu wa pango kwenye nyumba za Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), wakiwamo watumishi wa umma, wako hatarini kutimuliwa kutokana na malimbikizo ya madeni yanayofikia Sh. bilioni 10.

Imeelezwa kuwa wadaiwa hao walioko kwenye majengo hayo nchi nzima, walipewa notisi ya siku 14 itakayoisha Julai 5, mwaka huu, huku wakala ukiwataka waondoke mara moja vinginevyo utawafikisha mahakamani.

Kaimu Mkurugenzi Idara ya Umiliki TBA, Said Mdemu, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuwa mikataba yote waliyoingia na wateja wao ilikoma Juni 30, mwaka huu.

Mdemu alisema wapangaji wao, wakiwamo watumishi wa umma, taasisi na waliopanga kwa shughuli za biashara, wanatakiwa kulipa madeni yao kabla ya dalali aliyekabidhiwa suala hilo, Yono Auction Mart, kuwaondoa kwa nguvu kwenye majengo hayo.

"TBA imedhamiria kuwafikisha mahakamani wadaiwa hawa, wapo watumishi ambao wamekwishapoteza sifa ya utumishi, wastaafu, waliofariki dunia, waliofukuzwa pamoja na watumishi waliohamia vituo vipya vya kazi, wakabidhi nyumba, hatuna mkataba nao tena," Mdemu alisema.

Alisema TBA imejipanga kukusanya malimbikizo ya madeni ya mwaka wa fedha uliomalizika juzi na kuboresha mfumo wa ukusanyaji kwa kuwatumia wateja wao ujumbe mfupi wa maandishi kwa njia ya simu kuwakumbusha fedha ya pango.

Alisema wadaiwa hao kutokana na kudaiwa kwa muda mrefu, hawataingia tena mkataba wa upangishaji na TBA na kwamba baada ya notisi kuisha, wadaiwa watatangazwa majina yao kwenye vyombo vya habari na mali zao kukamatwa.

"Waajiri wa watumishi wa umma waliohamishwa vituo vya kazi wakiwa na madeni, wawasaidie kuhakikisha madeni yanalipwa ndani ya muda tulioutoa, mahitaji ya nyumba ni makubwa hivyo waondoke tuwapangishe wenye uhitaji," Mdemu alisema.

BISMILAH RAHMAN RAHIM



Familia ya marehemu **Dk. Omar Ali Juma** inapenda kuwakaribisha kwenye Hitima ya kumuombea Marehemu Dk. Omar Ali Juma itakayofanyika siku ya Alhamisi tarehe **4 Julai, 2019** saa kumi jioni katika Msikiti wa Ngazija.

Kufika kwenu ndio mafanikio yetu. Ndugu, Marafiki na Jamaa wote mnakaribishwa.

Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi.

**AMIN.**

615303502

# Makali ya kunguni nyumbani, shuleni -2

Katika toleo letu la jana tuliona jinsi wadudu aina ya kunguni wanavyosababisha usumbufu kwa taasisi hisisan shule za bweni na majumbani. Katika sehemu hii ya pili na ya mwisho, waathirika wanaendelea kusimulia, taarifa mbalimbali za utafiti na kauli ya serikali.

Agnes Moses (siyo jina lake halisi) anasimulia kuwa mmoja ya watoto wa ndugu yake walipata matatizo akawekwa moja ya mahabusu (anaitaja) jijini Dar es Salaam baada ya kutoka alifikia nyumbani kwake, Mikocheni.

Alisema baada ya kijana huyo kukaa siku chache na baadaye kuondoka, wakati wakifanya usafi kwenye chumba alichokuwa akilala, walikuta idadi kubwa ya kunguni.

"Tumeshatumia dawa za kila aina, kuna dawa ambayo tuliambiwa ndiyo kiboko kutoka Afrika Kusini, tulinunua tukatumia kuwaangamiza, lakini baada ya muda hali imerejea. Tunachofanya sasa ni kupiga dawa na kutoa magodoro na viti nje kila siku, lakini bado wapo," alisema.

Aliongeza: "Kunguni akiingia ndani ni kero huwezi kummaliza, gharama tuliyotumia ni zaidi ya milioni, lakini hatujafanikiwa, ukikaa kwenye kochi wapo, vyumbani wapo."

Alisema kutokana na changamoto hiyo anaogopa kutembelewa ndugu, jamaa na marafiki au wao kwenda kwao kwa kuhofia kuwasambaza.

### JESHI LA POLISI LAFUNGUKA

Akitolea ufafanuzi kuhusu malalamiko ya baadhi ya mahabusu kudaiwa kuwa na kunguni, Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, David Misime, aliliambia gazeti hili kuwa ofisi zote za serikali zina utaratibu wa kupulizia dawa za kuua wadudu mara kwa mara.

"Utaratibu uliopo kila siku asubuhi mahabusu husafishwa tena siyo kwa maji, wanasafisha kwa kutumia maji yenye dawa ili kuua wadudu pamoja na hao unaowataja. Pia upo utaratibu wa kupulizia dawa ya kuua wadudu 'fumigation' baada ya muda fulani ili kuondokana na maambukizi ya magonjwa kwa sababu sehemu hizo huingiwa na watu wa aina tofauti tofauti," alisema.

### SERIKALI YATOA HOFU

Naibu Waziri wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, aliliambia Nipashe kuwa kunguni haambukizi magonjwa kwa binadamu zaidi huleta maudhi.

"Kimsingi, kunguni ni wadudu ambao kitaalamu siyo vijidudu vinavyosababisha magonjwa, lakini kama wataalamu wa afya tunaona ni mdudu anayeleta maudhi, anapokuuma unawashwa unajikuna.

Aliongeza: "Mtu anapowashwa sana anajikuna na akijikuna sana, anaweza kupata maambukizi mengine ya ngozi ambayo sasa inaweza kumletea mtu madhara zaidi. Lakini kunguni kama mdudu siyo vijidudu vinavyosababisha magonjwa."

Dk. Ndugulile alibainisha mdudu huyo anahusishwa masuala ya usafi wa mazingira ya mtu binafsi na kubainisha kuwa kama yatakuwa machafu uwezekano wa mdudu huyo kuwapo ni ukubwa.

"Unapokuwa na mazingira safi basi kunguni siyo rafiki wa usafi, unapoona sehemu ina kunguni maana yake hali ya usafi hairidhishi. Nitumie fursa hii kutoa rai kwa jamii, shule na maeneo mengine kuhakikisha mazingira yetu wakati wote yanakuwa masafi," alisema.

Dk. Ndugulile alibainisha kuwa wadudu hao hupenda kujificha kwenye kuta zenye nyufa, chaga za vitanda, magodoro na maeneo mengine yasiyo na mwanga.



Naibu Waziri wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile

"Kama ukiona una tatizo la kunguni jitahidi vitu vyako uvitoe nje uvianike kwenye jua, hakikisha unatumia maji ya moto kufua matandiko, kuanika madogoro juani na kupulizia dawa, lakini kikubwa zaidi ni kuzingatia usafi na nyumba zenye nyufa zizibwe," alisema.

Kuhusu utafiti ambao umefanyika hadi sasa ambao unabainisha kuua kunguni kirahisi kwa sumu, Dk. Ndugulile alisema siyo kweli na kueleza kuwa zipo kemikali ambazo zinaweza kutumika kuwaangamiza.

"Siyo kila dawa unayoitumia inaua mdudu, kwa sababu viumbe hivi vimeumbwa kwa utofauti na hali ya upokeaji wake wa dawa, ni vizuri mtu anayesumbuliwa na kunguni apate ushauri kwa washauri wataalamu ili upate njia sahihi ya kuwaua," alisema.

### UTAFITI DUNIANI

Utafiti uliofanywa kuhusu mdudu huyu umekuja na matokeo kuwa, wanaweza kustahimili kupuliziwa dawa nyingi ya sumu kwa kuimarisha uwezo wake wa kujikinga dhidi ya sumu moja baada ya nyingine.

Mdudu huyo ameonyesha ana uwezo mkubwa wa kibaiolojia ya kujikinga dhidi ya sumu kali na kadri vizazi vya kunguni vinavyopuliziwa dawa yenye sumu ndivyo wanavyoimarisha uwezo wao wa kuzuia maafa miongoni mwa watoto wao.

Taarifa iliyochapishwa katika jarida la utabibu la The Journal of Medical of Entomology, watafiti wanasema vipimo 1000 vya sumu kali aina ya (neo-nicotinoid) vinahitajika kuua kunguni mmoja huko Marekani katika majimbo ya Cincinnati na Michigan ikilinganishwa na maeneo mengine duniani.

"Kuna hatari kubwa ya mdudu huyu kuenea kote duniani kutokana na utandawazi na soko huria ambao umefanya ulimwengu kuwa kitongoji kikubwa tu," watafiti hao wanabainisha.

Wanasayansi hao wanashauri kutafutwa mbinu mpya tofauti ya kukabiliana na wadudu hao badala ya kutumia sumu, kutafuta wadudu wengine wanaoweza kuwala ilikuzuia kunguni kuenea duniani kote.

### RANGI WAZIPENDAZO

Watafiti nchini Marekani baada ya kufanya uchunguzi wa kina, wamebaini kunguni hupenda baadhi ya rangi kushinda nyingine.

Uchunguzi uliofanywa na watafiti hao umebaini wadudu hao hupenda rangi nyeusi na nyekundu na huchukia njano na kijani kibichi.

Matokeo ya utafiti huo ambayo yalichapishwa katika jarida la kimatibabu la Journal of Medical Entomology, watafiti hao wanasema bado ni mapema kubaini iwapo shiti za rangi ya njano zinaweza kutumiwa kuwafukuza wadudu hao kitandani au la.

Daktari Corraine McNeill na wenzake walitaka kubaini iwapo rangi zinaweza kuathiri maeneo wanayovamia na wadudu hao.

Katika uchunguzi wao walitumia vibanda vidogo vya rangi mbalimbali kwenye maabara na kuchunguza kunguni ndipo alipobaini wanapenda rangi hizo mbili.

"Hata hivyo, baada ya uchunguzi, sababu kuu tuliyobaini iliwafanya kupenda rangi nyekundu ni kwa sababu kunguni wenyewe huonekana wakiwa wa rangi nyekundu, hivyo hudhani rangi hiyo ni kunguni wenzao," walibainisha watafiti.

Utafiti uliofanywa awali umebainisha kwamba rangi hizi pia hazipendwi na wadudu wengine wafyonza damu kama mbu.

### MWONEKANO WAKE

Kwa wasiomjua, kunguni ni mdudu mdogo mwenye miguu sita, kulia mitatu na kushoto mitatu na hawezi kuruka kama mende, hutambaa na huishi kwa kutegemea damu kama chakula chake ndiyo maana amekuwa msumbufu kwa watu.

Wadudu hawa wapo wa aina nyingi, wanaouma popo tu na wapo wanaowauma binadamu.

Kihistoria wadudu hawa walikuwapo enzi na enzi, lakini mwaka 1940 walimalizwa katika nchi zilizoendelea kama Marekani na za Ulaya, lakini ilipofika mwaka 1995 walirudi upya.

Sababu za kurudi kwao zinatajwa ni dawa za kuwaua ziliwatengenezea usugu, hivyo kukosa nguvu ya kuwaangamiza, kupigwa marufuku dawa hizo baada ya kuthibitika zina madhara kwa binadamu na huweza kusafiri nchi moja hadi nyingine.

Mdudu huyo hutaga yai kila siku kuanzia yai moja hadi matano na baada ya yai anakuwa mdogo mwenye milimita 1.5, kisha hukua hatua kwa hatua hadi anafikia kuwa kunguni kamili.

### TABIA ZA KUNGUNI

Mara nyingi mdudu huyu amekuwa na tabia ya kujificha hasa nyakati za mchana kwenye maeneo ambayo siyo rahisi kugundua kama wapo na hushamiri na kuonyesha makeke yao nyakati za usiku watu wakiwa wamelala.

## Polisi yakuta bunduki 6 zilizotelekezwa

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

SIKU chache baada ya Watanzania tisa kuuawa kikatili mpakani mwa Tanzania na Msumbiji na watu wanaosadikiwa kuwa ni magaidi, Jeshi la Polisi mkoani Ruvuma limeendesha msako na kukamata bunduki sita aina ya gobole zilizotelekezwa na watu wasiojulikana.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, ACP Simon Marwa, alitoa taarifa hiyo wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake mjini hapa kuhusu matukio mbalimbali ya kihalifu yaliyotokea mkoani humo.

Kamanda Marwa alisema kuwa kuanzia Juni 23 hadi 27, jeshi hilo liliendesha msako mkali na jumla ya bunduki sita zisizo na namba aina ya gobole zilizotengenezwa kienyeji zilikutwa zimetelekezwa katika maeneo mbalimbali zikiwa katika ofisi za vijiji vya Mpepo, Kihurunga na Liparamba vilivyopo katika kata ya Mpepo na Liparamba wilayani Nyasa mpakani mwa Tanzania na Msumbiji.

Kamanda alisema katika msako huo waliwatia mbaroni watuhumiwa kadhaa akiwamo Hassan Selemani (47), aliyekamatwa Juni 27 majira ya saa 7.00 usiku akiwa na meno manne ya tembo yenye uzito wa kilogramu 13.

Pia Juni 29, majira ya saa 10 usiku katika Kijiji cha Magazini, kata ya Lusewa wilayani Namtumbo mkoani hapa, Rashid Komba (33), alikamatwa akiwa na mkia wa tembo aliouhifadhi nyumbani kwake, wenye thamani ya Dola za Kimarekani 15,000 sawa na Sh. 34,465,000.

Vile vile, jeshi hilo lilimkamata Hadrack Marekela (22), kwa tuhuma za kuvunja na kuiba Tv nne na raia wa kigeni kutoka Sri Lanka, Hamid Sally Ishrath Ibrahim(47) na Segu Mohamed Ruwaisi (63), wamekamatwa wakiwa na madini aina ya Sulphire yenye uzito wa gramu 8.3 waliyoyanunua bila ya kufuata utaratibu na kuyaficha ndani ya nyumba yao.

Pia mtuhumiwa Mohamd Ismail (22), alikamatwa na polisi akiwa na mtambo wa kutengenezea pombe ya moshi.




Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Khatib Kazungu, akigonga kengele kuashiria kuorodheshwa kwa hatifungani ya Kampuni ya Mikopo ya Nyumba (TMRC), toleo la pili katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) jana. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# NDC yajipanga kuondolea wakulima jembe la mkono

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Taifa la Maendeleo (NDC) limesema kuwa limelenga kuondoa jembe la mkono kwa wakulima kwa kuleta mradi wa kuunganisha na kusambaza matrekta nchini.

Mradi huo ambao utawawezesha wakulima watakaofika katika Viwanja vya Maonesho ya 43 ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba) kupata treka kwa mkopo kwa kutoa Sh. milioni tatu kama kianzio kisha fedha zingine kulipa kidogo kidogo mpaka atakapomaliza deni.

Akizungumza jana katika maonesho hayo, Mkurugenzi Mwendeshaji wa NDC, Prof. Damian Gabagambi, alisema mradi huo ni mpango kati ya Tanzania na Poland wenye lengo la kuwasaidia wakulima kuwaondolea jembe la mkono.

Alisema matreka hayo hupatikana kwa mkulima kutoa asilimia 25 ya fedha ya bei yake, lakini katika msimu huu wa Sabasaba wametoa ofa kwa wananchi kupata mkopo wa matreka kwa masharti nafuu kwa kuanza kutoa Sh. milioni tatu.

"Katika msimu huu wa Sabasaba, wananchi wanaohitaji matrekta kwa mkopo wataanza kutoa Sh.milioni tatu na watapatiwa trekta... fedha inayobaki watalipa kidogo kidogo ndani ya miaka miwili bila riba isipokuwa atakaposhindwa kulipa ndani ya muda huo, atalazimika kulipa kwa riba.

Tunamtaka atakayeomba treka kwanza aende kijijini kwake aandike barua ambayo itathibitishwa na mtendaji wa kijiji kisha ataipeleka katika ikathibitishwe na mtendaji wa kata na mwisho atapeleka kwa Mkurugenzi wa halmashauri husika, tunafanya haya yote ili tuweze kupata watu waaminifu wanaohitaji trekta hizi, alisema.

"Tunataka jembe hili la mkono libaki katika makumbusho ya Taifa kwa sababu tunapoelekea halitakidhi mahitaji," alisema.


NMB Karibu yako

TAARIFA KWA WATEJA NA UMMA KWA UJUMLA

Ndugu Mteja,

NMB itafanya mabadiliko katika viwango vyake vya sasa, rasmi kuanzia tarehe **31 July 2019.** Pamoja na mabadiliko haya, NMB itaendelea kuweka viwango nafuu kabisa kwa wateja wetu ili kutimiza lengo la kuwa benki pendwa zaidi Tanzania. Mwaka 2018, NMB iliendelea kuongeza matawi, NMB Wakala na huduma za ATM kufanya mahusiano ya kibiashara kuwa ya kuridhisha zaidi na kupatikana kwa wepesi zaidi. Na kwa mwaka 2019, NMB itaendelea kwa bidii kuhakikisha inakuapatia huduma bora zaidi.

Asante kwa kuchagua NMB na ushirikiano wako wa muda mrefu nasi unayoifanya NMB kuwa benki bora zaidi ya biashara Tanzania.

Kwa taarifa zaidi ya mabadiliko haya ya viwango vyetu usisite kuwasiliana nasi kupitia tawi letu lililopo karibu yako au kwa simu **0800 002 002** bure!

**Imetolewa na uongozi wa NMB**

www.nmbbank.co.tz

MABADILIKO MAKUU YA GHARAMA ZA KIBENKI KWA MWAKA 2019

| Maelezo ya Gharama | Sehemu ya Gharama | Gharama mpya katika TZS |
|---|---|---|
| Ada ya uendeshaji ya mwezi | NMB Mwanachuo Account | BURE |
| | NMB Wisdom Account | BURE |
| | NMB Bonus Account | BURE |
| | NMB Personal Account/TPDF Account | 1,000 |
| | NMB ChapChap Account | BURE |
| | NMB Chipukizi Account | BURE |
| | NMB Fanikiwa Account | 2,000 |
| | NMB Business Savings Account | BURE |
| | NMB Pamoja Acoount | BURE |
| Kuweka Fedha | Sarafu Ndogondogo (1,5,10 na 20) USD, GBP, EURO | 5% |
| Gharama ya kuhamisha Fedha na NMB Mobile kwenda Mitandao ya Simu | 1,000 - 4,999 | 1200 |
| | 5,000 - 9,999 | 1800 |
| | 10,000 - 19,999 | 2200 |
| | 20,000 - 29,999 | 2700 |
| | 30,000 - 49,999 | 3200 |
| | 50,000 - 79,999 | 4700 |
| | 80,000 - 99,999 | 6000 |
| | 100,000 - 199,999 | 7200 |
| | 200,000 - 299,999 | 7700 |
| | 300,000 - 399,999 | 8200 |
| | 400,000 - 499,999 | 8700 |
| | 500,000 - 699,999 | 9200 |
| | 700,000 - 899,999 | 9700 |
| | 900,000 - 1,000,000 | 10000 |

215302802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Diaspora wapewe moyo kufanya makubwa zaidi

**MARA** kadhaa baadhi ya watu wamekuwa wanaeleza umuhimu wa Watanzania wanaoishi ughaibuni maarufu kama Diaspora katika maendeleo ya nchi.

Hoja ambayo husisitizwa na watu hao wakiwamo viongozi wakuu wa taifa letu ni kuwa ushiriki wa Diaspora kama watahamasishwa na kuhamasika katika maendeleo ya nchi unaweza kuchangia nchi kupanda chati kiuchumi.

Faida ya kuwashirikisha ni kuwa wanaweza kuchangia kwa kuwekeza nchini katika sekta mbalimbali, wakiwa na nia nzuri kutokana na kuwa wao ni sehemi ya Tanzania.

Katika miaka ya karibuni tulianza kuona dalili kuwa Diaspora wameanza kuhamasika kutokana na kauli wanazozitoa za kuwa tayari kuwekeza nchini, na kuchangia kukuza uchumi wa nchi yetu.

Uamuzi wa serikali zetu mbili ya Jamhuri ya Muungano na ya Zanzibar kuendelea kuwahamasisha na kuwashawishi Diaspora kushiriki katika kukuza uchumi wa nchi yetu kumesababisha pamoja na mambo mengine kufanyika kwa mikutano yao kila mwaka nchini kwa lengo la kuzungumza masuala yao na nafasi yao katika maendeleo ya nchi.

Tayari wameshaanza kushiriki kwa kusaidia baadhi ya miradi ya kijamii pamoja na kuwekeza katika miradi ya kiuchumi na wanaendelea kujipanga kufanya mambo makubwa zaidi.

Tumepokea kwa furaha na moyo mkunjufu taarifa kuwa uongozi wa Jumuiya ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi (Diaspora) uko tayari kusimamia ujenzi wa daraja refu la kisasa lenye uwezo wa kuunganisha miji miwili ya Dar es Salaam na Zanzibar katika harakati za kuimarisha uchumi na mawasiliano.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo akiwa pia mjumbe wa kamati ya biashara Tanzania, Jonas Njao, akiiongoza timu ya wanajumuiya hiyo alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi.

Jonas alisema Diaspora imeanza harakati za maandalizi ya kufanya utaratibu wa kuziomba serikali zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Mapinduzi ya Zanzibar kuuridhia mradi huo mkubwa wa kimataifa utakaoweza kupunguza tatizo la ajira kwa kundi kubwa la Watanzania.

Alisema wataalamu pamoja na wafadhili wa ujenzi wa mradi huo wa kiuchumi wameshajitokeza na kinachosubiriwa kwao kwa sasa ni kukubalika kwa maombi ya mradi ambao bado umekuwa adimu ndani ya Bara la Afrika.

Kwamba fursa wanazozipata za kuwasiliana na taasisi na kampuni wanazozunguka katika mataifa tofauti duniani zimelenga kutafuta nafasi za ajira zitakazosaidia kuimarisha ustawi wa wananchi kutokana na vijana wao kujikomboa katika masuala ya ajira.

Tunaishukuru na kuipongeza jumuiya ya Diaspora kwa kuona fursa hiyo, ambayo itatengeneza fursa za ajira kwa wingi pamoja na fursa kubwa na ya kipekee na ya kusaza ya miundombinu.

Kujengwa kwa daraja hilo itakuwa ni historia katika bara la Afrika, na kwa hakika kutasaidia kurahisisha usafiri wa wananchi na bidhaa pande zote kutoka upande mmoja kwenda mwingine badala ya kutegemea njia usafiri wa majini na wa angani, ambao umekuwa na changamoto nyingi.

Sekta nyingine ambayo itanufaishwa na mradi huo mkubwa na muhimu ni ya utalii, kwa kuwa watalii wengi watavutiwa kuja kuangalia kivutio hicho.

Tunazishauri serikali zote mbili kuupokea mradi huo kwa mtazano chanya na kuuridhia haraka ili utekelezaji wake uanze mara moja na kuinufaisha nchi yetu kujamii na kiuchumi, huku huku jitihada endelevu zikiendelea kuwahamasisha na kushawishi Watanzania wanaoishi ughaibuni kuendelea kushiriki katika ujenzi wa uchumi wetu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Raphael Kibiriti

# Serikali iwezeshe kununuliwa pamba ya wakulima nchini

**ILI** kuhalalisha tulonge yangu, ninaanza kwa kuitalii Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 hadi 2020.

Kimsingi Ilani hiyo inasisitiza vipaumbele vinne ambavyo ni pamoja na vita dhidi ya rushwa na ufisadi, kutengeneza ajira na kuendeleza kwa kiwango cha juu hali ya ulinzi na usalama wa taifa letu.

Lakini kipaumbele cha nne ni kuendeleza vita dhidi ya umaskini nchini, ambayo ndiyo mada ya leo.

Vita dhidi ya umaskini ni moja ya vipaumbele vilivyoko katika Ilani ya CCM, na kwa namna hiyo, tija yoyote inayogusa ustawi wa Watanzania walio wengi nchini, nikimaanisha wakulima, si ya kuiweka kapuni.

Kwa hivi sasa kuna kilio ambacho kinazidi kuripotiwa karibu kila siku na vyombo vya habari, cha wakulima wa pamba kutoka maeneo mbalimbali, wakiwa hawajui hatima ya pamba yao ambayo wameihifadhi majumbani mwao.

Wanaendelea kuihifadhi kwasababu hawana cha kufanya kwa kuwa hakuna kampuni ama wanunuzi wa zao hilo waliojitokeza kuinunua, pamoja na msimu wa ununuzi kuzinduliwa kutoka Mei 2, mwaka huu, takribani miezi miwili sasa.

Muungwana amekwishaandika tena juu ya kadhia hii inayoendelea kudidimiza wakulima wa pamba kiuchumi, kwa kuwa matarajio yao yanaonekana kutolipa hadi sasa.

Na hii ni baada ya jitihada kubwa walizozifanya za kuongeza tija katika uzalishaji kutokana na hamasa ya wadau, serikali ikiwamo.

Cha kusikitisha hata baadhi ya wakulima waliopeleka pamba yao kwenye Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS), wakitarajia itanunuliwa, wameambulia kuorodheshwa majina katika baadhi ya maeneo kwa ahadi kwamba watalipwa fedha zikija.

Kuna tukio la pamba kupakiwa kwenye magari ili iondoshwe katika moja ya maeneo mkoani Simiyu, bila ya wakulima kulipwa fedha zao.

Ni bahati kwamba wakulima walishtuka mapema na hivyo kuzuia magari, wakitaka kwanza walipwe fedha zao.

Taarifa zinasema hatua yao hiyo ilipata nguvu baada ya Mkuu wa Wilaya kuingilia kati na kuagiza pamba hiyo isichukuliwe hadi pale wakulima watakapolipwa fedha zao.

Aidha, mkuu huyo akaagiza pamba ya wakulima isikopwe kwa namna yoyote bila ya kununuliwa kwa fedha taslimu na kwa bei elekezi ya Sh. 1,200.

Liko pia tukio la baadhi ya wakulima waliopeleka pamba yao kwenye vyama vya ushirika vya msingi kwa ajili ya kuiuza na wakaamua kurudi nayo nyumbani, baada ya kukuta hakuna fedha.

Hatua kama hii ina athari ya moja kwa moja kwa mkulima, kwa maana ya ubora wa pamba yake.

Kwamba inaposafirishwa kwa tela ya kukokotwa na maksai kwa mfano kutoka nyumbani kwenda AMCOS na kisha kurudishwa nyumbani tena, ubora unaathirika.

Kwamba kuna masuala ya vumbi la njiani kwenda na kurudi, suala la kushusha na kupakia tena, hivyo kuathiri zaidi pato la mkulima huyu na dhana nzima ya kupambana na umaskini, kama inavyobainishwa kwenye Ilani ya CCM.

Kimsingi matokeo ya wakulima kutonunuliwa pamba yao hadi sasa, yanakwamisha jitihada za kuboresha maisha yao.

Muungwana anasema hivyo akiwa ni mtu anayetoka Kanda ya Ziwa na hivyo anaelewa maendeleo ambayo hupatikana kwa mtu binafsi, kaya na maeneo mbalimbali ya Kanda hiyo, pale msimu wa pamba unapozinduliwa na wakulima kuuza pamba yao.

Mbali na kutimiza majukumu yao kama ya kulipia ada na mahitaji ya shule kwa watoto, kipindi hiki huwa ni cha kuboresha makazi, kununua vyombo vya usafiri, mifugo na rasilimali zingine.

Muungwana anaendelea kutoa rai kwa serikali yetu sikivu kuwasaidia wakulima hawa kwa sababu kampuni za ununuzi wa pamba zinaonekana kama 'zina kamgomo' ambako sababu zake hazijawa wazi.

Nimesema kupambana na umaskini ni moja ya vipaumbele vya Ilani ya CCM, na kwa maana hiyo kununua pamba ya wakulima hawa ni muhimu katika dhima nzima ya kupambana na adui huyo.

HABARI KITAIFA

# Serikali kujenga miundombinu kimondo

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeahidi kujenga miundombinu ya kudumu katika kituo cha Kimondo Mbozi kwa ajili ya maonyesho ili kuhamasisha na kukuza utalii kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alisema hayo jana alipokuwa akifunga Maadhimisho ya Siku ya Kimondo Duniani yaliyofanyika kwa siku tatu katika kijiji cha Ndolezi mkoani Songwe.

Alisema shabaha ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kukuza na kuendeleza utalii kusini.

Kanyasu alitaja miundombinu itakayojengwa kuwa ni mabanda ya kudumu, viwanja vya michezo, jengo la kupokelea watalii, hali itakayosaidia kituo hicho kuwa na miundombinu bora ya utalii katika ukanda huo.

Mbali na miundombinu hiyo, alisema itaangalia uwezekano wa kulipa fidia kwa wananchi ili kuongeza ukubwa wa eneo litakalotumika kwa ajili ya shughuli za utalii kama vile kuanzisha bustani ya wanyamapori hai.

Alisema mkakati wa serikali ni kuyafanya maonyesho hayo yawe ya kudumu na yenye hadhi ya kitaifa na baada ya halmashauri kulipima eneo hilo, taasisi za wizara zitashiriki katika uwekaji wa miundombinu hiyo.

Naibu Waziri pia alisema uwapo wa kimondo hicho ni fursa kwa wananchi kujipatia kipato kutokana na watalii kutembelea kituo hicho.

Alisema wizara yake imelikabidhi eneo hilo la kimondo kwa Mamlaka ya Eneo la Ngorogoro (NCAA) ili kuchagiza utalii na jukumu la msingi la mamlaka hiyo ni kuhakikisha inatengeneza miundombinu bora kwa ajili ya utalii.

"Tunataka eneo hili la Kimondo mtalii yeyote atayefika aone ngoma za asili na vitu vingine vya kiutamaduni vitakavyomvutia ili kuona kwa muda mrefu.




Meneja wa Bidhaa za Intaneti wa Tigo, Mkumbo Myonga (kushoto), akionyesha kwa waandishi wa habari simu mpya za Smartphone aina ya TECNO S3 na TECNO R7, wakati wa uzinduzi uliofanyika katika viwanja vya Sabasaba jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Meneja Uhusiano wa kampuni ya TECNO Mobile, Eric Mkomoya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia kufungua maonyesho Sabasaba

**Na Elizabeth Zaya**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, leo anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF).

Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, alisema jana kuwa jumla ya nchi 35 zinashiriki katika maonyesho hayo.

Alisema maonyesho hayo kwa mwaka huu yatakuwa na utofauti mkubwa kwa kuwa ndiyo fursa ya Tanzania kujipambanua katika kujenga uchumi wa viwanda, mkakati ambao ndiyo chachu ya kufikia uchumi wa kati.

INAENDELEA UK.26

# Vitambulisho vya wajasiriamali vyatumika visivyo

**Na Ahmed Makongo, BUNDA**

BAADHI ya wajasiriamali waliopewa vitambulisho vya serikali kwa ajili ya kufanyia biashara bila usumbufu wa kutozwa ushuru katika Wilaya ya Bunda mkoani Mara, wamedaiwa kwenda kinyume cha kusudio la serikali.

Imedaiwa kuwa baaadhi ya wajasiriamali hao, wamekuwa wakiviazimisha vitambulisho hivyo kwa wafanyabiashara wenzao ambao hawana lengo la kukwepa kutozwa kodi na ushuru mbalimbali.

Hilo linadaiwa kufanyika kutokana na vitambulisho hivyo kutokuwa na picha ya mhusika, jambo ambalo ni rahisi kwa mjasiriamali asiyekuwa mwaminifu kumwazimisha mfanyabiashara mwenzake ambaye hana.

Hayo yalielezwa jana na baadhi ya madiwani kwenye kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

Diwani wa Namhura, Jogoro Amon (Chadema), alisema kutokuwa na picha ya mhusika kwenye kitambulisho, kunasababisha baadhi ya wajasiriamali kufanya mchezo huo, hususan kwenye maeneo ya minada na magulio.

"Vitambulisho hivyo baadhi ya wajasiriamali wanawapatia wenzao maana havina picha ya mhusika, ni bora wangeleta vingine vyenye picha," alisema Amon.

Kutokana na hali hiyo, alishauri serikali kulitazama suala hilo vizuri kwa kuwa baadhi ya wajasiriamali hao siyo waaminifu, licha ya serikali kuona umuhimu huo wa kuwatengenezea vitambulisho ili wasisumbuliwe katika kutozwa ushuru.

Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Lydia Bupilipili, alisema ni lazima kila mjasiriamali mwenye mtaji mdogo apewe kitambulisho cha serikali na si vinginevyo na kwamba mpango wa serikali si kuwakomoa wananchi wake bali ni kuwaondolea kero mbalimbali ikiwamo ya kutozwa ushuru kwa wenye biashara ndogo ndogo.




# Mfanyabiashara adaiwa kutekwa

INATOKA UK.2

**KAULI YA POLISI**

Alipoulizwa na Nipashe jana mchana kuhusu tukio hilo, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alisema suala hilo ni dogo na ameshamruhusu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kipolisi Konondoni kulizungumzia.

"Hili suala ni dogo, nimeshamruhusu Kamanda wa Polisi Kinondoni alizungumzie tangu mwanzo, mtafute yeye umuulize," Mambosasa alisema.

Alipotafutwa na Nipashe kulizungumzia, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Musa Taibu, alikiri jeshi hilo kupokea taarifa kutoka kwa Zitto aliyelieleza kuhusu alikohisi Ongangi amefichwa.

"Taarifa hizi alizileta Jumamosi na askari wangu waliondoka na Zitto hadi kwenye eneo ambalo alidai anahisi Ongangi ametekwa, baada polisi kufika walifanya ukaguzi maeneo hayo lakini hawakumkuta," Kamanda Taibu alidai.

Kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi alidai kuwa hadi sasa, jeshi hilo halijathibitisha kama taarifa za kutekwa kwa mfanyabiashara huyo ni za kweli ama la kwa kuwa limezipokea kutoka kwa Zitto.

Hata hivyo, Kamanda Taibu alisema jeshi hilo linaendelea na uchunguzi kuhusu tukio hilo.

Oktoba 11, mwaka jana saa 11 alfajiri, mfanyabiashara maarufu, Mohamed Dewji 'Mo', alitekwa na watu wasiojulikana kwenye Hoteli ya Colosseum iliyoko Oysterbay jijini alikokwenda kufanya mazoezi kwenye gym ya hoteli hiyo kisha kuachiwa usiku wa kuamkia Oktoba 20.

Baada ya kupatikana kwa Mo ikiwa ni siku tisa tangu kutekwa kwake, Jeshi la Polisi lilieleza kuwa alipatikana akiwa ametelekezwa ndani ya gari eneo la Viwanja vya Gymkhan jijini.



Mkurugenzi mstaafu wa Mamlaka ya Uendelezaji Biashara nchini, (TANTRADE), Jacquline Maleko (kushoto), akizungumza wakati akipatiwa huduma na Mkurugenzi wa Banda la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, (PSSSF), Eunice Chiume, (katikati) na Ofisa Malipo wa Mfuko huo, Nyangi Masalu, kwenye Maonyesho ya 43 ya Biashaya ya Kimataifa ya Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHAWETU.**

# Msekwa, Zitto wafunguka Lissu kuvuliwa ubunge

INATOKA UK 2

ubunge kwa kosa la utoro," Msekwa alisema.

"Sio kwamba sikujua walipokuwa, nilijua wapo Zanzibar wamesusia na kwa vile hawakuomba ruhusa, ikabidi waadhibiwe kwa mujibu wa Katiba.

"Kwa hiyo, siyo hoja kusema kuwa Spika hajui Lissu aliko, anaweza kujua lakini utaratibu wake unataka ufuatwe huwezi kujua kupitia magazeti."

Wakati Msekwa akiyasema hayo, Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo (Zitto) alisema jijini Dar es Salaam jana kuwa chama chake kitashirikiana na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kuchukua hatua dhidi ya uamuzi uliotolewa na Spika Ndugai.

Zitto alidai suala la Lissu lilitakiwa kupelekwa katika Baraza la Maadili kabla ya kufikiwa kwa uamuzi wa kumvua ubunge kwa kuwa chombo hicho hufanya kazi kama mahakama.

"Ilitakiwa Sekretarieti ya Maadili imshtaki Lissu kwenye Baraza la Maadili, baraza hili lishughulikie hiyo kesi ya Lissu ndiyo litoe hukumu.

"Na mtakumbuka watu kama kina (William) Ngeleja walipelekwa Baraza la Maadili, kuna utaratibu na siyo tu kwamba hujapeleka fomu unaondolewa," Zitto alisema.

Juzi, Chadema ilitangaza kuwa itakwenda mahakamani kupata tafsiri ya kisheria kuhusu sababu zilizotolewa na Spika Ndugai kumvua Lissu ubunge wa Jimbo la Singida Mashariki.

Ilielezwa na chama hicho kuwa Lissu bado yuko Ubelgiji akiendelea na matibabu yake ya kibingwa na anatarajia kurejea nchini Septemba 7, mwaka huu, tarehe ambayo mwaka 2017, alishambuliwa kwa kupigwa risasi zaidi ya 30 na watu wasiojulikana jijini Dodoma.

# Shahidi ataja damu kesi ya Mbowe

INATOKA UK. 3

Konstebo Fikiri alikuwa anavuja damu nyingi kichwani.

Madai hayo aliyatoa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba, wakati akisikiliza ushahidi wa Jamhuri dhidi ya vigogo tisa wa Chadema.

Jopo la Jamhuri liliongozwa na Mawakili wa Serikali Wakuu Faraja Nchimbi, Paul Kadushi, Dk. Zainabu Mango, Mawakili wa Serikali Jacqueline Nyantori, Wankyo Simon na Salimu Msemo.

Akiongozwa na Wakili Msemo, shahidi alidai kuwa Februari 16, mwaka jana, alikuwa kazini zamu ya usiku.

"Saa 5:40 usiku nikiwa wodi ya wazazi alikuja muuguzi wa zamu akaniarifu nahitajika kitengo cha dharura. Nilipokwenda niliwakuta wagonjwa wawili mmoja akivuja damu, huku akipiga kelele za maumivu na mwingine akiwa anaweweseka hana fahamu," alidai.

Aliongeza katika ushahidi wake kuwa: "Niliwaagiza wauguzi wawachome sindano za maumivu, nikamhoji aliyekuwa anatokwa damu kichwani, Fikiri kimetokea nini, akanieleza walikuwa wanatuliza maandamano ndipo wakajeruhiwa.

"Nilipojaribu kumhoji Rahim alikuwa anaweweseka na kuonyesha maumivu kwenye shingo upande wa kulia," alidai Dk. Alfani ni daktari wa Hospitali ya Polisi Barabara ya Kilwa ambayo ni ya rufani kwa zahanati zote za polisi.

Alidai kuwa baada ya kuwakagua majeruhi na kujiridhisha aliagiza wapelekwe wodini na walilazwa mpaka Februari 18, mwaka jana waliporuhusiwa. Pia alidai kuwa baada ya Rahimu kuendelea kulalamika maumivu aliagiza akafanyiwe kipimo cha CT Scan.

Baada ya maelezo hayo, shahidi huyo alihojiwa na wakili wa utetezi, Peter Kibatala kama ifuatavyo;-

**Kibatala:** Saa 5:40 usiku ulimhudumia nani?

**Shahidi:** Sikusema nilimhudumia mtu, muda huo niliitwa na muuguzi.

**Kibatala:** Kitu gani cha muhimu kilikufanya ukumbuke muda wa kuwahudumia majeruhi?

**Shahidi:** Kilichonifanya nikumbuke ni kumbukumbu ya tukio.

Kibatala: Februari 16, 2018 ulihudumia wagonjwa wangapi?

**Shahidi:** Nilihudumia wagonjwa wanne.

**Kibatala:** Hao wawili wengine unakumbuka muda uliowahudumia?

**Shahidi:** Nakumbuka.

**Kibatala:** Koplo Rahim alipata fahamu mbele yako?

**Shahidi:** Ndiyo alipata fahamu mbele yangu.

**Kibatala:** Uliagiza Koplo Rahim afanyiwe uchunguzi, umeitoa ripoti kama kielelezo cha kesi hii?

**Shahidi:** Sijatoa.

**Kibatala:** Ripoti ya CT Scan inasemaje?

**Shahidi:** Mimi niliagiza akapimwe na jukumu la ripoti ni la mgonjwa kwa hiyo sijui kama alikwenda au la. naeleza nilichokifanyia kazi.

**Kibatala:** Ni kweli kuwa aliumia shingoni peke yake?

**Shahidi:** Ndiyo.

**Kibatala:** Kwa ushahidi wako Koplo Rahim alikuwa amezimia iambie mahakama katika ushahidi wako ulizungumza chochote kuhusu fomu namba tatu ilikufikiaje?

**Shahidi:** Hapana.

**Kibatala:** Shahidi, wewe ndiye ulitoa ruhusa ya kutoka hospitali Koplo Rahim?

**Shahidi:** Hapana daktari mwingine.

**Kibatala:** Uliwahi kujua Koplo Rahim alikuwa wapi muda wote?

**Shahidi:** Sijui.

**Kibatala:** Kuna kanuni yoyote askari akiumia lazima apelekwe hospitali ya jeshi la polisi?

**Shahidi:** Hapana.

**Kibatala:** Kitabibu askari amezimia Mwananyamala utaagiza apelekwe hospitali ya karibu au?

**Shahidi:** Inategemea uamuzi wa mgonjwa au familia.

**Kibatala:** Ulisema Konstebo Fikiri ulimkuta anavuja damu kivipi?

**Shahidi:** Ndiyo na damu ilikuwa inadondoka matone chini.

**Kibatala:** Shahidi, nini madhara ya mtu kuvuja damu kwa muda wa saa tano?

**Shahidi:** Anapata madhara.

INAENDELEA UK. 26

HABARI MIKOANI

# Mwalimu mmoja afundisha shule nzima wanafunzi 366

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MWALIMU wa Shule ya Msingi Mikwa Kata ya Mapamba Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, Elias Zabron, ameiomba serikali kuongeza walimu hasa wa masomo ya sayansi katika shule hiyo yenye zaidi ya wanafunzi 366 na mwalimu mmoja.

Shule hiyo ilianzishwa na wazazi baada ya wanafunzi waliokuwa wakisoma katika Shule ya Msingi Mapamba kuwa mbali kwa zaidi ya kilometa 15, huku baadhi walilazimika kwenda kusoma katika shule za msingi zilizopo Halmashauri ya Uyuwi mkoani Tabora.

Zabroni aliyabainisha hayo alipotembelewa na maofisa kutoka mpango wa kuinua ubora wa elimu Tanzania (EQUIP) kukagua ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi moja ya walimu vilivyokuwa vikijengwa kwa fedha kutoka katika mfuko huo.

Alisema shule hiyo ina zaidi ya wanafunzi 366, madarasa matatu na ofisi moja ya walimu huku ikiwa na wanafunzi kuanzia darasa la awali mpaka la tatu na kudai kuwa amekuwa akiwafundisha kwa awamu, hivyo kusababisha wengi wao kutojua kusoma na kuandika.

Aidha, Zabron, alisema akifundisha siku moja siku inayofuata anajikita katika kusahihisha madaftari ambayo huchukua siku tatu hadi kumaliza, na siku zote hizo wanafunzi wanakosa masomo na kuendelea kucheza nje hadi mwisho wa vipindi.

"Shule hii ina zaidi ya wanafunzi 366 kuanzia darasa la awali hadi darasa la tatu na nimekuwa nikifundisha mwenyewe, na wakati mwingine nawapatia vitabu wanafunzi wa darasa la tatu wenye uelewa na kwenda kufundisha darasa la kwanza na awali," alisema Zabron.

Aliongeza: "Kulikuwa na mwalimu mmoja wa kujitolea na alikuwa analipwa shilingi 500 na kila mzazi mwenye mtoto, lakini ameshindwa kuendelea kufundisha kutokana na kutolipwa kwa zaidi ya miezi mitatu, na ninapoumwa hata ikichukua miezi miwili wanafunzi wanakosa masomo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu, Michael Matomora, alikiri shule hiyo kuwa na mwalimu mmoja ambae anafundisha kuanzia darasa la awali hadi la tatu, na kuongeza kuwa mwezi huu ataongeza walimu wengine watatu ili kwenda kusaidia ufundishaji.

Aidha, alisema shule hiyo ni moja kati ya shule shikizi zilizosajili na kuwa shule za msingi kamili baada ya EQUIP kujenga vyumba viwili vya madarasa na ofisi moja ya walimu katika Shule ya Msingi Mikwa, Kawekamwe na Mliza.



Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti (kushoto), akimsikilia mkulima wa kahawa jinsi kahawa inavyopimwa baada ya kuzindua msimu wa ukusanyaji kahawa Nkwenda wilayani Kyerwa. Nyuma yake aliyevaa fulana ya kijani ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Japhet Justine. **PICHA: MPIGAPUCHA WETU**

## Prof. Mahalu ataka mazingira bora wahitimu elimu ya juu

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MAKAMU Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino (SAUT), Balozi Prof. Costa Mahalu, ameiomba serikali kuandaa mazingira bora kwa wahitimu wa elimu ya juu, kwa kuwapa mikopo stahiki.

Ametaka mikopo hiyo kupitia asasi za selikali kama benki ili waweze kutumia ujuzi walionao, hasa kiujasiriamali ili kuleta maendeleo kwa mtu binafsi na taifa kwa ujumla.

Prof. Mahalu alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari juu ya chuo hicho kuadhimisha miaka 20 na kuelekea 25 tangu kianzishwe mwaka 1998 ifikapo leo.

Aidha, Mahalu na uongozi wa Saut, waliishauri serikali na sekta binafsi kuwatumia wasomi katika mipango ya maendeleo ya nchi.

"Wasomi ni wengi na ajira ni chache ambapo ukosefu wa ajira kwa wananchi wengi walio wasomi ni changamoto kubwa kwa serikali, hivyo sisi kama Saut tunaishauri serikali iweke utaratibu wa kuwakopesha wasomi ambao hawajapata ajira," alisema.

Vile vile Prof. Mahalu aliwaomba wananchi wawe mstari wa mbele kuwekeza katika elimu ya juu kwa kufadhili miradi ya maendeleo, badala yasio kuwaachia watu wa nje au nchi jirani kuwekeza katika elimu.

Naye mratibu wa sherehe ya maadhimisho hayo, ambaye ni mhadhili wa Saut, Tiitus Ngapemba, alisema Saut imefanikiwa kuongeza matawi mapya 13 katika kanda mbalimbali nchini, ikiwa ni kufikisha /kusogeza huduma ya elimu ya juu karibu na jamii, na imeongeza udahili wa wanafunzi kutoka 204 hadi 11,400 kwa mwaka wa masomo 2018/2019 na kwa mwaka wa masomo 2012/2013 udahili ulikuwa wanafunzi 13,121.

# Kahawa wahakikishiwa malipo wakati mwafaka

**Na Mwandishi Wetu,** KAGERA

MSIMU wa ukusanyaji wa kahawa kwa mwaka 2019/2020 kutoka kwa wakulima hadi vyama vya msingi umezinduliwa rasmi mkoani Kagera,

huku Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ikiwahakikishia wakulima wa zao hilo kupata malipo yao kwa wakati.

Katika msimu uliopita Benki ya Maendeleo ya Kilimo ilitoa zaidi ya shilingi bilioni 30 ambazo ziliwanufaisha moja kwa moja wakulima 148,000.

Akizungumza baada ya kuzinduliwa msimu wa ukusanyaji wa kahawa ambapo vyama vikuu vya ushirika vya KCU 1990 na KDCU kutangaza malipo ya awali kuwa shilingi 1,100 kwa kilo moja ya maganda, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, amesema benki yake itatoa fedha kwa wakati na kumfikia mkulima moja kwa moja kupitia mfumo wa benki.

"Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alizindua akaunti jumuishi za wakulima ili wakulima wasikatwe fedha zao hata kama ni senti moja ilipwe moja kwa moja kwa mkulima na sisi kama TADB tutahakikisha tunalipa fedha hizo kupitia akaunti za benki," alisisitiza Justine.

Justine aliwathibitishia wakulima kuwa TADB imejipanga kimkakati kuhakikisha kuwa wakulima wananufaika na kuwapo kwa benki ikiwamo kupata malipo yao kwa wakati na kumudu kununua pembejeo za kilimo.

"Kama Benki ya Maendeleo ya Kilimo hapa nchini, tumejipanga kuchagiza mageuzi katika sekta ya kilimo ili kufanikisha azma ya Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Rais John Magufuli ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025," alisema.

Akizindua rasmi msimu huo wa ukusanyaji wa kahawa hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti wilayani Kyerwa Nkwenda, aliwahakikishia wakulima serikali imejipanga kuondoa changamoto zote zilizojitokeza msimu uliopita na mkulima atanufaika na kahawa yake na kulipwa kwa wakati.

Akiongea na wakulima wa kahawa na wananchi waliokusanyika kumsikiliza Nkwenda Kyerwa alisema kuwa tayari vyama vikuu vya ushirika mkoani Kagera tayari vimepewa Sh. bilioni saba na TADB, aidha, wakulima ambao tayari wamekusanya kahawa yao kwenye vyama vya msingi wataanza kulipwa malipo ya awali ya 1,100/- kwa kila kilo kuanzia jana.

"Msimu huu tutahakikisha kuwa wakulima wanalipwa fedha zao kwa wakati ikiwa ni pamoja na kuhakikisha fedha hizo hazipiti katika mikono mingi ya viongozi wa vyama vya msingi," alisema na kuongeza kuwa mkulima atalipwa fedha zake moja kwa moja kupitia akaunti yake.

Katika kuondoa changamoto za msimu uliopita wa mwaka 2018, Brigedia Gaguti alikikagua Chama cha Msingi Rwabwere na kujionea namna ya kupima kahawa za wakulima na kuagiza kuwa lazima kilo zote na pointi ziandikwe na mkulima ili kupunguza malalamiko. Kuhusu fedha za wakulima, Mkuu wa Mkoa huyo alisema fedha hizo zisitolewe maamuzi na viongozi wa vyama vya msingi bali wakulima wenyewe ndiyo waamue zitumike zifanye nini.

Aidha, Brigedia Gaguti na ujumbe wake walikagua pia shamba bora la mkulima Abdu Ndegeza na kuona kahawa bora na zilizokomaa zikivunwa. Tayari Chama Kikuu cha Ushirika cha KDCU Limited tayari kimekusanya kilo 3,200,000 matarajio yake ni kukusanya kilo 35,000,000.

# Mtoto anusurika kuuawa Dar akidhaniwa ni mchawi

**Beatrice Moses**

MTOTO wa kiume anayetajwa kuwa na matatizo ya akili mwenye umri wa miaka minane amenusurika kuuawa na wananchi wenye hasira akidhaniwa kuwa ni mchawi.

Mtoto huyo jina linahifadhiwa, alikutwa akiwa mlangoni mwa nyumba ya mkazi wa Makondeko Temboni Kata ya Saranga, wilayani Ubungo jijini Dar es Salaam, huku akiwa uchi usiku wa manane.

Taharuki ilizuka juzi saa 9 usiku baada ya Agness Miyeji kueleza kuwa alishtuka baada ya kusikia sauti ya paka akilia katika hali iliyomshangaza, hivyo akamwamsha mumewe wakaanza kusali.

"Ajabu ikatokea wakati tunasali ile sauti ikawa inazidi kusikika kama inafuata kwenye mlango, ndipo mume wangu akalazimika kwenye kufungua mlango ndipo tukamkuta mtoto wa kiume akiwa uchi kasimama mlangoni," alisema mama huyo.

Alieleza kuwa kitendo hicho kiliwapa hofu wakaamsha baadhi ya majirani, kisha wakashauriana kwenda kwa mjumbe wa eneo lao liitwalo Makondodeko, ambapo pia waliona kaptula wakamvalisha mtoto huyo.

"Mjumbe aliwasiliana na polisi jamii wa Saranga ambapo walifika hata hivyo, mtoto hakuweza kujieleza chochote kila alipohojiwa alikuwa kama vile anaweweseka tu, wakawasiliana na viongozi wa msikiti jirani ili watangaze kama mtu kapotelewa na mtoto ambaye alichukuliwa na kwenda kuhifadhiwa kwenye ofisi ya ulinzi shirikishi Saranga," alisema.

Hata hivyo mama wa mtoto huyo (Ester Hurra) alifika kwenye ofisi hiyo akiwa ameongozana na baadhi ya jirani zake ambapo baada ya kuhojiwa na polisi jamii alieleza kuwa mwanaye ana matatizo ya akili anatibiwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

"Nilikwenda kwenye mkesha kwenye kanisa la Sabato lililopo jirani na nyumbani kwangu nilimwacha mwanangu amelala na kaka zake, lakini niliporejea saa 11 alfajili sikumkuta, kaka zake walikuwa wamelala fofofo," alisema mama wa mtoto huyo.

Alibainisha kuwa hali hiyo ilimtisha akawaamsha na kuwahoji hakuna aliyejua mtoto amekwenda wapi, ndipo akawashirikisha wenzake aliokuwa ameongozana nao kutoka kwenye mkesha wakaanza kumtafuta kwa kuuliza kwa majirani, lakini hakuna aliyekuwa amemuona.

Kutokana na taarifa za kukutwa akiwa mtupu polisi jamii walishauriwa mtoto huyo kuchunguzwa na mzazi ili kujiridhisha kama hajafanyiwa vitendo vya kikatili ikiwamo kulawitiwa, ilithibitika kuwa yu salama.

"Katika kushauriana majirani wengine walishauri tuwashirikishe polisi jamii kumtafuta, mmoja alipopiga simu alijulishwa kuwa kuna mtoto amekutwa huko Makondoke, jamani mwanangu huyu ni mgonjwa anatibiwa Muhimbili na pia nampeleka hata kwenye maombi siyo mchawi," alisema mama huyo.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Saranga, Godwin Muro, alifika kwenye ofisi hizo za ulinzi shirikishi huku akiwa na hofu.

"Nimetumiwa ujumbe kwenye simu nikashtuka na kukimbilia hapa kwa pikipiki, huku nikiwaza juu ya usalama wa mtoto kwa sababu najua kuna wananchi wenye tabia ya kujichukulia sheria mkononi... nilihofia wasije kuwa wamemjeruhi au kumuua, mimi namfahamu huyu mtoto kweli ana matatizo, bora amepatikana akiwa mzima," alisema Muro.




Mwendesha bodaboda akiwa ameisheheni mzigo wa mkaa katika eneo la Kibamba jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# 'Serikali haijazuia utafiti mbegu GMO'

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imesema utafiti kuhusu mbegu za Teknolojia ya Uhandisi Jeni (GMO), haujawahi kuzuiwa wala kuchoma moto majaribio yake yanayofanyika hapa nchini bali unaendelea kufanyika kwa baraka zote za serikali na utakapokamilika maamuzi yatatolewa.

Majaribio ya utafiti wa mbegu za GMO yanafanyika katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo cha Makutupora kilichopo mkoani Dodoma, kuhusu mbegu za mahindi na Taasisi ya Utafiti Mikocheni iliyopo jijini Dar es Salaam, kuhusu mbegu za mihogo.

Kauli ya serikali ya kuendelea na utafiti wa mbegu za GMO imekuja ikiwa takribani miezi minne iliyopita kufuatia Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Mhandisi Mathew Mtigimwa, kueleza uamuzi wa serikali kusitisha utafiti huo unaofanyika katika taasisi hizo mbili za utafiti.

Akizungumza katika mjadala wa wazi wa siasa za uchumi wa GMO kwa Tanzania uliofanyika katika ukumbi wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mratibu wa Utafiti wa Bioteknolojia za kilimo Tanzania kutoka Taasisi ya Kilimo Tanzania (TARI), Dk. Fred Tairo, alisema kwa sasa utafiti huo unaendelea na upo katika hatua mbalimbali katika vituo hivyo.

Alisema TARI haijaacha kufanya utafiti wa GMO tangu ilivyoanza na unaendelea na umeonyesha matokeo chanya kwa mbegu zote mbili.

Dk. Tairo, alisema watu pamoja na vyombo vya habari nchini walielewa vibaya kuhusu taarifa zilizotolewa na kwamba serikali ilitaka watafiti wafuate utaratibu wa kutoa matokeo waliyokuwa wanayapata kwenye majaribio hayo ili kuondoa mkanganyiko.

Mtafiti huyo alisema msimamo wa serikali ni kuendelea na utafiti wa GMO ili uweze kukamilika katika hatua zake muhimu na kisha utakapokamilika utapeleka katika mamlaka husika kwa ajili ya kutoa maamuzi.

# Serikali yakubali ombi kanisa kuongezewa masafa ya redio

**Na George Tarimo,** IRINGA

SERIKALI imekubali ombi la Kanisa Katoliki la kuomba kibali cha kuongeza masafa yao ya Fm kwa maeneo ambayo hayafikiwi huduma hiyo.

Kauli hiyo ilitolewa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, kwenye maadhimisho ya miaka 23 ya kuanzishwa kwa Redio Maria nchini kwenye ibada ya misa takatifu katika kiwanja vya Kichangani mjini hapa.

Sambamba na maadhimisho hayo, Prof. Ndalichako aliongoza harambee ya kuchangia chombo hicho ili kiweze kujiendesha ambapo kwa Julai zinahitajika zaidi ya Sh. milioni 90.

"Nimesikia changamoto zenu kuhusiana na masafa na redio kutofika kwa baadhi ya maeneo, naomba niwahakikishie yote ambayo mmesema kwenye risala ambayo yanahusika na masuala ambayo labda yanahitaji kuwezeshwa na vyombo vya serikali...mimi kama serikali nimeyapokea, nitayafikisha mahala husika ili yaweze kufanyiwa kazi," alisema Ndalichako.

Waziri Ndalichako aliwashukuru waumini wa Kanisa Katoliki kwa maombi yao ambayo wanamwombea Rais John Magufuli pamoja na serikali yake ambayo yamemwezesha Rais kufanya mambo makubwa ambayo wengi walikuwa wakiyaogopa kwa sababu yanahitaji uthubutu.

"Rais amekuwa mstari wa mbele kutetea wanyonge, kulinda rasilimali ambazo zilikuwa zinaporwa na watu ambao walikuwa hawalitakii mema taifa, lakini kwa ujasiri wake ameweza na nchi inashuhudia makubwa," alisema.

Waziri huyo amepongeza chombo hicho kwa kufanya vizuri katika tume kwa sababu siku za hivi karibuni amekuwa akishuhudia baadhi ya vyombo vya habari vikikemewa kwa kukiuka maadili na miiko pamoja kutozingatia sheria kanuni na taratibu, lakini hajawahi kusikia Redio Maria ikipewa onyo.

Rais wa Redio Maria Tanzania ambaye ni Mwenyekiti wa Marafiki wa redio hiyo, Hamphrey Shira, akisoma risala yao, alisema redio hiyo ni chombo cha uinjilishaji chenye lengo la kufikisha habari njema kwa wokovu na watu wote kila wakati na kwa uharaka kupitia teknolojia mbalimbali za mawasiliano hususan ya redio.

Shira alisema kuwa changamoto kubwa wanayokumbana nayo ni uhitaji mkubwa sana toka majimbo yote ambayo hayafikiwi na masafa yao ya FM wote, licha ya kuomba wafikishiwe.

Katika maadhimisho hayo, wanakusudia kukusanya fedha kwa ajili ya uendeshaji wa kawaida wa Sh. milioni 90 kwa mwezi Julai ili waweze kukidhi mahitaji yao.

Katika ibada hiyo iliongozwa na Rais mstaafu wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC) ambaye pia ni Askofu wa Jimbo la Iringa, Tarcisius Ngalalekumtwa.

# Aapa kupambana na wizi wa mifugo

**Na Zanura Mollel,** ARUSHA

KAMANDA wa Kikosi cha Kuzuia Wizi wa Mifugo Mkoa wa Arusha, Yusuph Sarungi, amekemea vikali wizi wa mifugo kwa wakazi wa Wilaya ya Longido mkoani hapa na kuwataka kufanya biashara kwa uaminifu kwa kufuata taratibu za nchi.

Akizungumza mwishoni mwa wiki na wafanyabiashara wa mifugo kwenye mnada wa MIVRAF ulioko Kijiji cha Eworendeke, Sarungi alisema kumekuwa na malalamiko ya baadhi ya wafanyabiashara juu ya wachungaji wa mifugo inayoletwa mnadani hapo kuiba mifugo wakiwa malishoni.

"Nimepokea taarifa ya wachungaji waliopata ajira za kuchunga mifugo wakati inasubiri kusafirishwa kwenda Kenya, kuiba mifugo. Unakuta mchungaji amepewa mbuzi au ng'ombe 100 akachunge, akirudisha kutoka malishoni anarudi na 98, " alisema Sarungi.

Alisema wizi ni kosa kisheria na hata sasa wameshabainika wanaofanya matukio ya wizi. Alisema upelelezi ukikamilika watachukuliwa hatua kisheria kwa kujihusisha na wizi na utoroshaji wa mifugo kwa kuwa wanaikosesha serikali mapato.

"Majina tunayahifadhi kwa ajili ya kukamilisha upelelezi. Ukiibiwa mfugo wako toa taarifa kwa wakati katika kituo cha polisi kilichoko jirani," alisema Sarungi.

Aliwataka wote wenye tabia ya kubadilishana stakabadhi ya malipo kwa ajili ya mifugo kwenda nje ya nchi kwa lengo la kukwepa kulipa kodi waache mara moja tabia hiyo kwa kuwa kitendo hicho hakina tofauti na mtu anayehujumu uchumi wa nchi.

"Unakuta stakabadhi imeandikwa jina la John, lakini anayesafirisha mifugo anaitwa Shabani. Haiwezekani, mbaya zaidi tarehe ya kusafirisha mifugo ni tofauti, inaonyesha ni udanganyifu umetumika acheni hiyo tabia," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Mifugo katika soko hilo, Saruni Laizer, alisema wameshaweka mikakati ya kuwadhibiti wale wote wanaotuhumiwa kuwa wezi wa mifugo kwa sababu vitendo vya wizi vinachafua jina la soko.

"Hawa wachungaji wa mifugo tutawadhibiti. Tumeshakubaliana na viongozi wa serikali ya kijiji hapa soko lilipo. Tumejipanga vizuri na hatuko tayari kuona serikali inapoteza mapato kwa ajili ya wachache," alisema Laizer.

Alisema kwa sasa mtu yeyote atakayefika kuomba kazi ya kuchunga mifugo katika soko hilo, atatakiwa kupita kwenye ofisi ya viongozi wa soko kwa ajili ya kujiandikisha ili litakapotokea tatizo lolote abanwe ipasavyo.

"Ni lazima na si ombi, wachungaji wa mifugo kupitia ofisini tuwasajili na kuwatambua ndipo tuwape kazi. Hatuko tayari kufanya kazi na wezi wa mifugo," alisema Laizer.



Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqqaro, wakati alipokuwa akizindua kituo kipya cha Maktaba ya Jamii cha Madecha kilichojengwa katika Kata ya Sinoni kwa thamani ya zaidi ya Sh. milioni 40 chini ya ufadhili wa familia ya Mathew Hladezuk (17) kutoka nchini Marekani. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## Watakiwa kuhamasisha watoto kupenda kujisomea

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WANANCHI mkoani Arusha wametakiwa kuhamasisha watoto kupenda kujisomea vitabu mbalimbali kwenye maktaba, ili kuepuka vishawishi na matendo yasiyofaa ikiwamo kuvuta bangi na ubakaji. Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, alisema hayo jana wakati akizindua kituo kipya cha maktaba ya Jamii cha Madecha kilichojengwa katika Kata ya Sinoni kwa thamani ya zaidi ya Sh. milioni 40 chini ya ufadhili wa familia ya Mathew Hladezuk (17) kutoka Marekani.

Daqarro, mbali na kumpongeza mwanzilishi wa kituo hicho, Prof. Richard Msomba na mkewe, Elaine Msomba, alisema iko haja kwa kila mzazi kumhamasisha mtoto wake kujisomea vitabu mbalimbali katika maktaba hiyo, jambo litakalosaidia kuongeza uelewa katika masomo yao.

"Vijana wa Kata ya Sinoni watumie maktaba hii kujiendeleza kielimu na serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo kwani vijana wetu wakihamasika vizuri kujisomea itapunguza matukio ya uhalifu," alisema.

Awali, Prof. Msomba ambaye ni mwalimu wa uchumi nchini Marekani, alisema kituo hicho kitahudumia bure wanafunzi wa chekechea hadi kidato cha sita.

Alisema ameamua kujenga maktaba hiyo yeye na mke wake, ikiwa sehemu ya mchango wao kwa jamii katika kuendeleza sekta ya elimu baada ya kubaini kuwa jamii haina huduma hiyo na watoto wengi wanajisomea nyumbani na kukosa sehemu ya utulivu.

"Maktaba hii itahudumia shule mbalimbali za sekondari na msingi zipatazo 17 na wanafunzi wapatao 140 wanajisomea kwa kila siku na wakati wa mitihani wanafunzi wanakuwa wengi zaidi," alisema Prof. Msomba.

# NGO zamwangukia JPM mabadiliko ya sheria

**NA Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MASHIRIKA yasiyo ya kiserikali (NGO) yamemwomba Rais John Magufuli asitie saini muswada wa sheria ya uendeshaji mashirika hayo na kampuni zisiyotengeneza faida na taasisi zinazosimamiwa na wadhamini uliopitishwa na bunge hivi karibuni kwani una upungufu mwingi.

Aidha, yamesema akiutia saini ukawa sheria, madhara hayatakuwa kwa mashirika hayo pekee bali pia itawaumiza wananchi wengi ambao hupatiwa huduma na mashirika hayo.

Pia sheria hiyo itaziathiri taasisi mbalimbali za kimataifa na za kikanda zinazoendesha shughuli nchini, mashirika hayo yameahidi kufikisha suala hilo Jumuiya ya Afrika Mashariki, (EAC) na Bunge la Afrika Mashariki (EALA).

Viongozi wa mashirika hayo waliyasema hayo juzi jijini hapa walipokutana kwa ajili ya kujadili sheria hiyo, ambayo hawakupata fursa ya kuijadili kwa kuwa ilipelekwa bungeni kwa hati ya dharura.

Akichangia kwenye mkutano huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Haki Madini, Amani Mhinda, alisema sheria hiyo ikitumika kama ilivyopitishwa na Bunge itaathiri wananchi wengi.

"Kwa bahati mbaya haijagusa NGO pekee yake imezigusa na taasisi nyingine ambazo zimesajiliwa chini ya sheria mbalimbali kama vile Sheria ya Vyama vya Hiari, Sheria ya Kampuni na ile ya wadhamini ambazo zote zimejumuishwa chini ya NGO kwa bahati mbaya," alisema Mhinda ambaye pia ni mwanasheria wa haki za binadamu.

Alisema sheria hiyo itazilazimu taasisi zinazofanya kazi za kusaidia jamii ambazo hazitengenezi faida zilizosajiliwa kama kampuni na chini ya Bodi ya Wadhamini, zitatakiwa ndani ya miezi miwili ziwe zimejisajili kwa msajili wa NGO.

"Kuna umuhimu kupewa muda kutafakari athari kabla Rais hajatia saini na tunaomba tupate fursa kuendelea na mazungumzo haya, kuona sheria ambazo zinakinzana na hali ilivyo," alisema Mhinda.

Aliongeza kuwa: "Tunafahamu kulikuwa na udhaifu uliopaswa kurekebishwa, lakini unaweza kusababisha madhara mengine ya kisheria na kusababisha mashirika mengi kufungwa na kuathiri wananchi waliokuwa wakipatiwa huduma na mashirika haya."

Alisema kuna wengine walikuwa wanafadhiliwa kutoa elimu, elimu na huduma ya afya na pia wanapata tiba kupitia NGO na kwa muda ambao yamefanyika mabadiliko haya haijatoa fursa kwa watu wote kusikilizwa.

Naye Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali la Civic and Legal Aid, (CILAO), Odero Odero, alisema waathirika wakubwa wa sheria hiyo ni wanufaika wa huduma zinazotolewa na asasi hizo za kiraia, hivyo Rais akitia saini na kuanza kutumia itaathiri shughuli wanazoendelea kufanya kwa sasa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo.

"Endapo mashirika hayo yatakoma kufanya kazi, wananchi ndio watakaoumia zaidi, hivyo naamini serikali iko kwa ajili ya wananchi, itatusikia na itatoa muda zaidi wa majadiliano. Tukikaa pamoja tunaweza kujadili kuondoa changamoto zinazoweza kusababishwa na sheria hiyo, endapo Rais atatia saini kuanza kutumika," alisema Odero.

Naye Mtendaji Mkuu wa Chama cha Wanasheria wa Afrika, Donald Deya, ambaye ofisi zao ziko jijini Arusha, alisema sheria hiyo ina athari kwa taasisi za kimataifa zilizosajiliwa nchini, hivyo akasema bado uko mlango wa kuipinga mahakamani.

# Kuzorota soko la maziwa kwazua hofu

**Na Mary Mosha,** HAI

KUZOROTA kwa soko la maziwa yatokanayo na uwekezaji wa kisasa wa mifugo katika Wilaya ya Hai, kunaweza kuua ari ya wafugaji kuongeza tija ya uwekezaji katika sekta hiyo.

Hayo yalielezwa jana na Mratibu wa Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV), Isack Kitururu, wakati wa mafunzo ya namna bora ya uandaaji wa mpango mkakati wa uboreshaji wa masoko hasa katika uongezaji wa thamani.

Mafunzo hayo yameandaliwa na Jukwaa la Masoko na Mawasiliano la ABC BROS, kwa ushirikiano na SNV.

Kwa mujibu wa Kitururu, Mkoa wa Kilimanjaro soko la maziwa lipo, lakini katika kulikabili kwa kuandaa bidhaa bora bado imekuwa ni changamoto hali ambayo wameiomba serikali kuingilia kati suala la ubora wa bidhaa kabla ya kumfikia mlaji.

"Sisi kutokana na warsha tuliyoitoa leo ni dhahiri kuwa ni lazima kuwapo kwa soko la uhakika la kuchukua maziwa yote yanayozalishwa na wakulima kwa kuzingatia ubora, usafi na usalama," alisema Kitururu.

Akifungua warsha hiyo, Ofisa Mifugo na Uvuvi wa wilaya hiyo, Elia Machange, akimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, alisema, mpaka sasa wana uwezo wa kuzalisha lita milioni 36 kwa mwaka licha ya kuwa bado wana viwanda viwili pekee vya usindikaji wa maziwa yao.

Alisema kwa sasa wanashirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali ili kuhakikisha vyama vya ushirika vya maziwa vinaundwa na maziwa yote yanafikishwa huko kwa ajili ya usalama wa afya za walaji na kuepusha madhara kwa binadamu.

"Kutokana na uzalishaji wetu hivi viwanda bado havitoshi... tunahitaji viwanda zaidi waweze kutusaidia kukusanya maziwa yote hayo kwa faida ya walaji...ingawa kunamwekezaji ambaye yupo tayari kuwekeza kiwanda chake mkoa wa jirani ambapo ametuhakikishia kukusanya maziwa yetu yote kutokana na kupata soko Uarabuni, " alisema Dk. Machange.

Mtaalamu wa sekta ya maziwa kutoka muungano wa vyama vya maziwa Mkoa wa Kilimanjaro (KDCJE), Benovila Balama, alisema bado wafugaji wanapaswa kuhamasishwa kutumia maziwa yaliyosindikwa ili kuepusha kutumia yenye vijidudu ambavyo vinaweza kusababisha magonjwa.

"Maziwa yanayotoka moja kwa moja kwa mfugaji kwenda kwa mlaji yanakabiliwa na changamoto nyingi kutokana na kutopimwa na kutofahamika mara moja kiwango chake cha usafi, hivyo nawashauri kujikita katika kuhakikisha wanatumia maziwa yaliyosindikwa ambayo ni salama kwa afya zao," alisema Balama.

Gema Kavishe ni mshauri wa mradi alisema lengo la kuanzishwa kwa mradi huo ni kuhakikisha wanawajengea uwezo wazalishaji, wasindikaji na walaji wa bidhaa za maziwa lengo likiwa kuzalisha zenye bora, salama na safi za maziwa kwa ajili ya kuingia kwenye ushindani wa soko la kimataifa na kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja, mkoa na taifa kwa ujumla.

"Uchunguzi unaonyesha vipo vyama vya msingi vya kupokea maziwa kwa ajili ya kupimwa, lakini 1/4 ndio yanayopelekwa kwenye chama ni 3/4 huuzwa mtaani bila kufanyiwa vipimo jambo ambalo ni hatari kwa afya za walaji," alisema Gema.

Baadhi ya wauzaji wa maziwa, Dismas Mfuru, mkazi wa Bomangombe, aliomba serikali kuangalia namna ya kutoa elimu endelevu kwa wasindikaji wa maziwa ili waweze kusindika maziwa freshi.

## Wakumbushwa kulipa ada ya uchimbaji visima

**Na Mary Mosha,** MOSHI

OFISA wa Maji wa Bonde la Mto Pangani (PBWO), Segule Segule, ametoa rai kwa wananchi ya mikoa ya Kanda ya Kaskazini kuanza kulipa sehemu ya ada ya umiliki wa visima vya maji ili wapewe ushauri wa kitaalamu kuhusu matumizi yake.

Alitoa rai hiyo jana wakati akizungumza na Nipashe kuhusu operesheni ya Wizara ya Maji kuwatambua wamiliki wa visima vya maji ambao hawajasajiliwa kwa mujibu wa sheria.

Segule alisema bado kuna changamoto kubwa ya ulipaji wa ada kidogo ya uchimbaji wa visima kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Maji, namba 11 ya mwaka 2009 kifungu cha 43.

Alisema kwa sasa wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu uchukuaji vibali wanapotaka kuchimba visima iwe ni kwa ajili ya maji ya matumizi ya nyumbani au ya viwandani au kilimo ili kupewa ushauri wa kina kutoka kwa wataalamu wa namna bora ya kuchimba bila kugusa maji taka.

"Tunawaomba wananchi kufika kwenye ofisi zetu kupata wataalamu watakaowawezesha kuchimba visima vyenye ubora kwa kuwa kuna umbali wa visima ambavyo haturuhusu, hivyo ni vyema wakafika kwa ajili ya ushauri," alisema ofisa maji.

Kutokana na wito huo, mmoja wa wakazi wa Mkoa wa Kilimanjaro, Aneti Samson, alisema hadi kufikia sasa hajaona umuhimu wa kuchimba kisima chake na kulipia hivyo aliiomba serikali kuongeza jitiada za kutoa elimu na kuonyesha kwa matendo matumizi ya fedha hizo zinapomrudia mwananchi.

Omary shabani, alisema ulipaji wa kiwango walichokipanga kingeweza kulipika ikiwa tu elimu ya kutosha ingetolewa kwa wananchi na ushauri hasa maeneo ya vijijini, ili kusaidia sintofahamu zilizotanda kwenye akili za watu kuwa hii ni njia pekee ya serikali kuchukua kodi kwa wananchi.



Mafundi wa Kampuni ya CRSG, wakiendelea na ujenzi wa barabara inayounganisha eneo la Kijitonyama na Sinza Uzuri, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

## Wamwomba RC kuingilia kati usalama wao

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WAKAZI wa Kata ya Karanga, Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, wamemwomba Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Anna Mghwira, kuingilia kati suala la ulinzi na usalama wa kata hiyo kutokana na kukithiri kwa matukio ya kihalifu huku viongozi wa kata wakishindwa kuwajibika.

Mmoja wa wakazi hao akizungumza na Nipashe, Mary Costantine, alisema kumekuwapo na matukio ya kihalifu yanayoongezeka katika kata hiyo huku wakiwatuhumu viongozi wa kata hiyo kujibu majibu ya jeuri na dharau mara wanapoenda kuomba msaada wa changamoto hizo.

Alisema matukio hayo ya kihalifu yamekithiri kutokana na ongezeko la vichaka virefu pembezoni mwa barabara licha ya kuwa kata hiyo ni miongoni mwa kata zilizopo katika Manispaa ya Moshi.

Ernest Msofe, alisema mbali na kuwapo kwa vichaka pembezoni mwa hizo, pia wapo watu ambao sio waaminifu wanaouza na kutumia dawa za kulevya kwa vijana.

"Tumechoka na matukio haya, katika kipindi cha mwezi mmoja uliopita, wapo baadhi ya kinamama wameporwa fedha na hata wengine kubakwa katika eneo la Kilimani, huku viongozi wa kata wakiwa wameufumbia macho uhalifu huo," alisema Msofe.

Shabani Mkure, alisema matukio mengine yanatokea natunapoenda kutoa taarifa katika uongozi wa kata wanayapuuzia kutokana na watendaji hao asilimia kubwa kutokaa katika kata hiyo na kushindwa kujua changamoto za kata.

"Sisi tunamwomba Mkurugenzi wa Manispaa kutupa mtendaji ambaye kwanza mwenye utayari wa kusikiliza kero za wananchi kwa wakati na ikiwezekana anayeishi katika kata hiyo, ili kujua uchungu wa matukio yanayotokea na kuchukua hatua kwa wakati," alisema.

Nipashe ilimtafuta Mtendaji wa kata hiyo, Leocardia Moswary ili kujibu changamoto zinazowakabili wananchi na kusema hayupo tayari kuzungunza kwa sasa.

Diwani wa Kata ya Karanga, Jonathani Makupa, alipoulizwa kuhusu changamoto hizo, alisema kwa sasa kwenye kata hiyo hakuna posili jamii, lakini amelichukua suala hilo na atalifanyia kazi kwa wakati.

HABARI MBEYA

# Elimisha kuwezesha jamii maisha ya furaha

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

SHIRIKA lisilokuwa la kiserikali linalowezesha utoaji wa taarifa zenye umahiri katika nyanja za uelimishaji, kujenga uwezo na kuleta matokeo chanya kwa jamii (Elimisha), limeanzisha mpango bunifu wa kuongeza thamani ya maarifa ili kuiwezesha jamii kufikia maisha yenye furaha.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Shirika hilo, Festo Sikagonamo, wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari, jijini Mbeya.

Sikagonamo alisema mpango unalengo la kuhakikisha kila mwananchi ana uelewa wa kutosha kuhusu matumizi ya bajeti kuanzisha ngazi ya familia hadi taifa, alisema watahakikisha wanaelimisha jamii kujua mapato na matumizi yanayopatikana ili kusaidia kufanya shughuli nyingine za maendeleo.

"Tumeamua kuanzisha mpango huu bunifu wa kimkakati ambao ni endelevu kwa lengo la kuhakikisha jamii inafikia furaha ya maisha kwa kufahamu mapato na matumizi yanayopatikana na hii itasaidia kila mmoja kufahamu anatumia kiasi gani cha fedha na anaingiza shilingi ngapi kwa siku, mkakati huu utamwezesha kila mmoja kuwa na matumizi sahihi ya fedha atakazokuwa anazipata," alisema Sikagonamo.

Alisema katika utafiti waliofanya kwenye mikoa ya Mbeya na Songwe, walibaini wananchi kuwa na uelewa mdogo kuhusu bajeti, wengi hawajui kiasi cha fedha wanachokipata na wanachokitumia, lakini pia hawana vipaumbele vya mahitaji yao badala yake mtu hununua au hutumia kitu pale anapokiona.

Aliongeza kuwa zipo faida mbalimbali zinazopatikana kwa sababu ya kuzingatia bajeti ambayo inahusisha mapato na matumizi miongoni ni kupunguza vitendo vya uhalifu vikiwamo rushwa na wizi kuanzia ngazi ya familia hadi taifa.

Ofisa Habari wa Shirika la Elimisha, Elizabert Nyivambe, alisema mwananchi akifahamu bajeti itakuwa rahisi kukuza uchumi wake, itamsaidia kupunguza mahitaji yasiyo ya lazima na itamletea faida pia kuongeza mapato kufungua ajira.

Alisema waathirika wakubwa wa matumizi ya bajeti ni vijana kwa sababu ya changamoto ya ajira na mitaji, baadhi yao hawana uelewa wa namna ya kubana matumizi kwa kiasi cha fedha kinachopatikana.

Alisema mpango huo bunifu wa kuongeza thamani ya maarifa kwa kutumia fikra bunifu ni kuiwezesha jamii kufikia maisha yenye furaha na utapunguza vichocheo vya umaskini miongoni mwa jamii.

"Mpango huu umelenga kuwafikia wanawake wajasiriamali na wakulima wenye ulemavu wa kusikia, waandishi wa habari na kila mwananchi mmoja mmoja anayefika katika ofisi zetu kwa ajili ya kupata ushauri wa kibajeti tunawashukuru wadau mbalimbali na serikali kwa kuunga mkono jitihada hizi," alisema Elizabeth.

## Wanandoa washauriwa kupanga uzazi kwa kipato

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

WANANDOA wameshauriwa kupanga uzazi wa mpango kwa pamoja ambao utasaidia kuamua ni lini waanze kuzaa, watoto wangapi, lini waache kuzaa kulingana na vipato vyao.

Rai hiyo ilitolewa jana na Meneja Utetezi kutoka Shirika la Advance Family Planning (AFP), James Mlali, alipozungumza na Nipashe kuhusua faida za uzazi wa mpango.

Alisema ni muhimu kwa wanandoa ambao ni mume na mke waliofika umri wa kuzaa, kukubaliana kuzaa idadi ya watoto wataoweza kuwatunza ili kumwezesha mama na mtoto kuwa na afya njema, pia kumsaidia mama kurudi katika hali yake ya zamani.

Alisema suala la uzazi ni nyeti kwa kuwa linahusisha masuala mbalimbali ikiwamo matumizi ya njia za uzazi wa mpango, wenza hukubaliana kutumia njia ya uzazi wa mpango wanayoiona inafaa ili kuzuia mimba zisizotarajiwa.

"AFP tumekuwa tukitoa mafunzo mbalimbali ya uzazi wa mpango lengo ni kuielimisha jamii kutambua umuhimu wa kutumia uzazi wa mpango ambao unahusisha matumizi sahihi ya njia za uzazi wa mpango, lakini pia wenza kupanga idadi ya watoto wao, tumepata malalamiko kadhaa kwa kinamama wakidai jukumu hilo wanaachiwa na waume zao," alisema Mlali.

Alisisitiza kinababa kushiriki kupanga uzazi wa mpango na wake zao badala ya kuwaachia jukumu hilo wenza wao ambao wakati mwingine hushindwa kufanya uamuzi wa idadi ya watoto watakaozaa.

Baadhi ya kinamama jijini Mbeya walilalamikia njia za uzazi wanazozitumia kama vile sindano, vidonge na vijiti kwa madai zinawaletea adha kwenye miili yao kama kunenepa kupita kiasi, kupata hedhi kwa kupindi kirefu na kutoshika mimba.

Walisema wanapoeleza changamoto hizo kwa madaktari hudai njia hizo hazina madhara badala yake zina maudhi madogo madogo na kuwasisitiza kuwa wavumilivu au kubadilisha aina nyingine ya njia ya uzazi wa mpango.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako (kulia), akisalimiana na Mkurugenzi wa Redio Maria Tanzania, Padre John Maendeleo, baada ya kuwasili katika adhimisho la misa ya miaka 23 tangu kuanzishwa kwa redio hiyo, katika viwanja vya Kichangani, Manispaa ya Iringa juzi. Wa tatu kushoto ni Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki, Jimbo la Iringa, Tarcisius Ngalalekumtwa. **PICHA: OFISI YA ASKOFU**

# Wanawake wajasiriamali kulindwa vitendo vya ukatili

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

ASASI isiyokuwa ya kiserikali inayotekeleza programu mbalimbali zinazolenga kuendeleza Sekta ya Kilimo kwenye masuala ya masoko, utawala bora na Sera (MIICO), imeanzisha programu maalum ya kumsaidia mwanamke mjasiriamali kupaza sauti (Sauti ya Mwanamke sokoni) ili kupinga vitendo vya mbalimbali vya ukatili.

Hayo yalisemwa juzi na Mkuu wa programu kutoka Asasi ya MIICO, Catherine Mulaga, wakati wa kikao cha kujadili changamoto zinazowakabili wanawake sokoni na kuweka mpango kazi wa namna ya kukabiliana nazo.

Alisema walianzisha programu hiyo ya Sauti ya Mwanamke sokoni baada ya kuwapo kwa changamoto mbalimbali zinazowakabili wanawake wajasiriamali wanaojitafutia riziki.

Pia alisema katika utafiti walioufanya kwenye sekta isiyo rasmi, walibaini changamoto ushiriki mdogo wa wanawake katika nafasi za uongozi sokoni jambo linalosababisha kushindwa kushughulikia masuala yao.

Alisema changamoto nyingine ni kushamiri kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia ambavyo husababisha wanawake kutukanwa, kudhalilishwa na uonevu pamoja na adha ya upatikanaji wa maji hali inayosababisha kinamama kupata shida wanapokuwa kwenye hedhi.

"Tumelenga kufikia masoko nane ikiwamo Illomba, Soweto, Mabatini Uyole na Uhindini katika Jiji la Mbeya kutoa elimu ya namna wanavyoweza kutambua haki zao na kuimarisha shughuli zao na kuongeza kipato," alisema Catherine.

Pia alisema watahakikisha wanawafikia wafanyabiashara wote walioko sokoni na kuwahamasisha kujiunga kwenye vikundi ili kuanzisha miradi ya pamoja, kukopesheka kwenye taasisi za kibenki na kupata mafunzo mbalimbali.

Ofisa Maendeleo wa Jiji la Mbeya, Magdalena Ngenzi, alisema Asasi ya MIICO imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha mwanamke anayefanya biashara zake sokoni anatimiza majukumu yake bila kupata changamoto.

Alisema asasi hiyo imewapa nguvu kinamama kujiamini na kufanya shughuli zake, lakini pia kuunganishwa na huduma za kisheria kutetea haki zao kutetea maslahi yao pindi wanapoonewa.





# Asilimia 12.3 ya kaya zina akaunti benki

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UTAFITI wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi kwa mwaka 2017/18, umeonyesha kuwa asilimia 12.3 ya kaya Tanzania Bara zina angalau mtu mmoja mwenye akaunti benki huku Dar es Salaam ikiongoza.

Sambamba na hilo, asilimia ya kaya zenye wanakaya wenye akaunti hizo ni kubwa mijini kwa asilimia 23.8, huku vijijini ni asilimia 6.1.

Kwa mujibu wa ripoti ya utafiti huo iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) mwishoni mwa wiki ambayo ilizinduliwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kaya zenye watu wenye akaunti zinatofautiana kimkoa huku Mkoa wa Kigoma ukiwa na asilimia 2.3 na Dar es Salaam asilimia 31.3.

Mikoa mingine na asilimia kwenye mabano ni Dodoma (9.1), Arusha (10.1), Kilimanjaro (11.4), Tanga (tisa), Morogoro (9.6%), Pwani (12.3), Lindi(13.4), Mtwara (15.4), Ruvuma (13.9), Iringa (12.3), Mbeya (11.1), Singida (tatu) na Tabora asilimia 12.

Mingine ni Rukwa (10.1), Shinyanga (7.7), Kagera (7.4), Mwanza (11.7), Mara (11.6), Manyara (5.6), Njombe (17.9), Katavi (4.4), Simiyu (7.6), Geita (7.3) na Songwe asilimia 11.

Kwa upande wa matumizi, utafiti huo umeonyesha kuwa mkoa wa Dar es Salaam wastani wa matumizi ya kaya kwa mwezi ni Sh. 720,946, huku Rukwa ikiwa na wastani wa chini wa Sh. 268,041.

Mwenendo huo, unaonekana pia katika wastani wa matumizi ya mtu mmoja mmoja ya chakula, bidhaa zisizo za chakula na matumizi yote ya mtu mzima mmoja kwa mwezi.

Kuhusu wastani wa mstari wa umaskini, matokeo ya utafiti huo yanaonyesha kuwa mwaka 2017/18 ni Sh. 33,748 kwa mtu mzima mmoja kwa mwezi na kwenye mahitaji ya msingi ni Sh.49,320.

Pia katika taarifa hiyo, inaonyesha kuwa kumekuwa na ongezeko la asilimia ya kaya zinazoishi katika makazi yaliyojengwa kwa vifaa vya kisasa kama vile zege, mawe, saruji na vyuma.

Kwa mwaka 2017/18 asilimia 84.1 ya kaya zinaishi katika nyumba zenye paa la kisasa ikilinganishwa na asilimia 68.0 ya kaya mwaka 2011/12.

Utafiti huo pia unaonyesha kuwa asilimia 78.8 ya kaya zinaishi kwenye nyumba zilizojengwa kwa kuta imara mwaka 2017/18 ikilinganishwa na asilimia 46 kwa mwaka 2011/12.

Vile vile, asilimia 50.1 ya kaya zinaishi kwenye nyumba zilizojengwa kwa sakafu imara mwaka 2017/18 ikilinganishwa na asilimia 40 mwaka 2011/12.

Katika matumizi ya umeme, asilimia 29.1 ya kaya zote zimeunganishwa kwenye umeme kupitia Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco).

Hili ni ongezeko la asilimia 11.1 kati ya mwaka 2011/12 hadi mwaka 2017/18, ambapo kaya sita kati ya 10 (63.2 za mijini zimeunganishwa, huku kaya moja kati ya 10 (asilimia 0.4) za vijijini.

Katika ripoti hiyo, inaonyesha asilimia 93 ya kaya zinatumia choo cha aina yoyote. Kati ya kaya hizo, asilimia 74.7 zinatumia vyoo visivyoboreshwa na asilimia 25.3 inatumia vyoo vilivyoboreshwa.

Matumizi ya vyoo vilivyoboreshwa ni mkubwa mijini ni asilimia 41.2 huku vijijini ni asilimia 16.



Meneja wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Kati, Antonio Manyanda, akiwaonyesha wadau wa mamlaka hiyo mkataba mpya wa wateja ambao unaelekeza haki na wajibu wa mteja na mamlaka katika mkutano ulifanyika jijini Dodoma mwisho wa wiki, kwa kuwashirikisha wadau kutoka mikoa ya Singida, Kigoma, Tabora na Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Dodoma yatenga hekta 2,000 viwanda Mtumba

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

JIJI la Dodoma limetenga hekta 2,000 katika eneo la Mtumba kwa ajili ya ujenzi wa viwanda mbalimbali, vikiwamo vya uchakataji maziwa ili kutengeneza bidhaa zitakanazo na maziwa.

Pia ujenzi huo utafanyika sambamba na kujenga vituo vya kukusanyia maziwa katika kila Halmashauri za Jiji la Dodoma, ili iwe rahisi katika upatikanaji wa maziwa.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Kessy Maduka, alisema jana jijini hapa kuwa Jiji la Dodoma huzalisha zaidi ya lita 11,000 za maziwa kwa mwaka, hivyo wawekezaji wanatakiwa kuchangamkia fursa katika sekta hiyo.

"Jiji limetenga eneo hilo kwa ajili ya viwanda, wawekezaji mnapaswa mjitokeze kuwekeza katika viwanda vya maziwa," alisema Maduka.

Alisema lengo la kutangaza fursa hizo mkoani hapa ni pamoja na kutaka kuifanya Dodoma kuwa jiji la biashara kama yalivyo majiji mengine kulingana na fursa ambazo zimetolewa wawekezaji mnapaswa kuzichangamkia.

Pia alisema kuna fursa ya ujenzi wa kiwanda cha kuchakata na kuongeza thamani ya alizeti na kuwataka wawekezaji kuchangamkia fursa hiyo.

Alisema katika kuhakikisha wanafanikisha uwekezaji katika eneo la Kondoa na Chemba zimetengwa hekta 2.8.

Alisema kutokana na fursa hizo wawekezaji wanapaswa kuangalia nini wanapaswa kuwekeza ili iwe rahisi kwao kuja kuwekeza katika Jiji la Dodoma kuinua sekta ya viwanda ambayo ni muhimu katika kuinua uchumi wa nchi.

# Ruwasa kumaliza tatizo la maji vijijini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKALA wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa), jana ulianza kazi rasmi ili kuondoa tatizo la muda mrefu la maji vijijini ambalo lilitokana na kukosekana kwa uendelevu wa miradi iliyojengwa.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema hadi Aprili, mwaka huu, jumla ya vituo vya kuchotea maji 131,370 vilijengwa vijijini ambavyo vilipaswa kuhudumia watu milioni 32.8 sawa na asilimia 83.8.

Hata hivyo, alisema kati ya vituo hivyo 86,700 sawa na asilimia 65.6 pekee ndivyo vinavyofanya kazi vikihudumia watu Milioni 25.3 sawa na asilimia 64.8 ya wananchi waishio vijijini.

Prof. Kitila alisema sekta ya maji vijijini inakabiliwa na usimamizi hafifu wa miradi ya maji. Miongoni mwa sababu ya hali hiyo inasababishwa na wahandisi wa maji kuwajibika kwa mamlaka zaidi ya moja.

"Ziko changamoto zingine za kiutendaji ambazo zimekuwa zikishughulikiwa kwa njia mbalimbali kwa mujibu wa sheria na kanuni za utumishi wa umma," alisema.

Prof. Kitila alisema ili kukabiliana na changamoto za kimfumo zinazoikabili sekta hiyo vijijini, Rais John Magufuli aliagiza watumishi wote wa maji wahamishiwe kwenye wizara hiyo.

"Tumeshafanya mchakato wa kisheria ambao umeanzisha wakala huu unaofanya kazi leo (jana), tunaimani utaweza kutatua changamoto nyingi za kimfumo zinazoikabili sekta ya maji vijijini," alisema.

Alitaja majukumu ya wakala huo ni kusanifu na kusimamia ujenzi wa miradi, kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi, kuchimba visima na kujenga mabwawa, kusajili na kuviwezesha vyombo vya watumiaji maji, kuhamasisha sekta binafsi kushiriki na kumshauri Waziri wa Maji kuhusu uendeshaji wa sekta za maji.

Naye, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Ruwasa, Gonsalves Rutakyamirwa, alisema watahakikisha wanafanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha matarajio ya serikali yanafikiwa.



## HABARI ZANZIBAR

# Bima yatakiwa kuelimisha jamii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UONGOZI wa Mamlaka ya Bima Tanzania umetakiwa kutoa elimu kwa jamii kukata na kutumia bima kutoka kwa watoa huduma waliosajiliwa na mamlaka husika, ili kuongeza pato la taifa pamoja na kudhibiti watu wanaoghushi huduma hiyo.

Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahmoud, alitoa wito huo wakati akizungumza na viongozi, wadau na wananchi katika maadhimisho ya Siku ya Bima Zanzibar yaliyofanyika katika Viwanja vya Kumbukumbu Kisonge Mjini Unguja.

Alisema endapo kampuni na wataalamu wa bima watakuwa na utamaduni wa kutoa elimu ya mara kwa mara, wananchi watapata uelewa umuhimu wa huduma ya bima na hawatasita kununua huduma hiyo.

"Kwa sababu mamlaka ya bima ni chombo cha ushauri kwa serikali kuhusu masuala ya soko la bima, ni matumaini yangu wananchi sasa watanunua huduma za bima, na endapo kutatokea migogoro au kutoelewana kati ya kampuni ya bima na mteja nina uhakika mamlaka yenu itakuwa tayari kulitatua na kulipatia ufumbuzi," alisema Ayoub.

Pia Mkuu wa Mkoa alisema serikali ya Mjini Magharibi inathamini jitihada za mamlaka za bima na wadau wake katika kuendeleza maendeleo ikiwa ni pamoja na kuwasogezea wananchi huduma za bima kupitia kampuni, madalali, mawakala na wakadiria hasara wanaosajiliwa na mamlaka hiyo.

"Kulingana na ripoti ya mwenendo wa soko la bima nchini ni dhahiri kwamba juhudi za mamlaka pamoja na wadau wote wa bima zinazaa matunda kwa ongezeko la ukuaji wa kiwango cha asilimia saba kwa sekta ya bima inaonyesha wazi kwa kushirikiana na wadau, mamlaka inafanya kazi kwa bidii kwa lengo la kukuza soko la bima nchini, amesema Mkuu wa Mkoa.

Ayoub alizitaka taasisi za serikali kuwa mstari wa mbele kuvikatia bima vyombo vyao ili kuenda sambamba na mabadiliko ya sheria na maelekezo ya serikali kuhusu matumizi ya bima kwa vyombo mbalimbali.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, Kamishna wa Mamlaka ya Bima Tanzania, Mussa Juma, alisema kuwa kila mwananchi ana haki ya kupata fidia endapo atapata ajali za barabarani zitokanazo na vyombo vya moto na lengo la maadhimisho hayo ni kutoa elimu ya bima kwa jamii na kuwapa miongozo ya kupata haki zao za bima pale watakapopatwa na ajali.

Alisema Mamlaka ya Bima imekuwa na mikakati mbalimbali ili kuhakikisha inaongeza wateja kwa kutumia sekta za kibenki zitakazotoa huduma za upatikanaji wa bima kwa gharama nafuu pamoja na kuzitaka kampuni zinazoingiza bidhaa chini kukata bima hapa Tanzania na si nje ya nchi kama ilivyokuwa zamani.

"Sasa hivi tumekuwa na utaratibu wa kuziagiza kampuni mbalimbali zinazoagiza bidhaa zao nje ya nchi kukata bima hapa nchini kwetu kwa mujibu wa sheria zilizopo na sio kule wanakoagiza biashara zao kama ilivyokuwa zamani," alisema Juma.

Vile vile, alisema kuwa mamlaka hiyo imekuwa na utaratibu wa kusaidia na kuchangia katika huduma za kijamii ikiwamo afya, elimu na watu wenye mahitaji maalumu kwa kutoa msaada wa mahitaji na vifaa mbalimbali kwa watu wenye mahitji maalum.

Kwa upande wake Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Kusimamia Bima Tanzania, Khadija Issa Said, alisema wamekuwa na mikakati mbalimbali ya kuhakikisha wanayafikia maeneo tofauti kutoa elimu kwa jamii na kuona wanapata uelewa wa kutosha na kuzitumia fursa zinazopatikana katika mamlaka zao.



Baadhi ya vibanda vya wafanyabiashara waliohamishwa eneo la Mwenge na kupelekwa kando ya Barabara ya Coca Cola, jijini Dar es Salaam jana, vikiwa vitupu kutokana na ugumu wa biashara katika eneo hilo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali yatambua mchango wa vyama vya wafanyakazi

**Na Rahmam Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema serikali inatambua kuwapo kwa vyama vya wafanyakazi nchini, kuendana na sheria na Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na mikataba ya kimataifa.

Akifungua Mkutano Mkuu wa Nne wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Zanzibar (ZATUC), uliofanyika mjini hapa, alisema serikali inatambua kuwa wafanyakazi na vyama vya wafanyakazi ni kundi muhimu ulimwenguni na ili mafanikio yaweze kupatikana kazini, ni lazima pawepo wafanyakazi walio tayari kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, nidhamu, uadilifu na uzalendo katika mazingira bora.

Alisema kutokana na hali hiyo serikali imekuwa ikiridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa pamoja na kutunga sheria na kanuni zinazohusiana na masuala ya wafanyakazi.

"Yote hayo yanafanywa kwa madhumuni ya kufikia malengo na kuhakikisha wafanyakazi wanatimiza majukumu yao katika mazingira yalio bora zaidi pamoja na kulinda maslahi yao, " alisema.

Alisema serikali imekuwa na mazingatio maalum ya wafanyakazi kwa kutambua kuwa wanahusiana moja kwa moja na ukuaji wa uchumi, ukiwa ndio msingi wa ustawi wa maisha ya wananchi.

Dk. Shein alisema serikali inazingatia umuhimu wa kuimarisha ushirikiano uliopo na vyama vya wafanyakazi kupitia ZATUC, ikiwa ni utekelezaji wa ilani ya CCM ya mwaka 2015-2020, ibara ya 139.

Pia, aliipongeza Jumuiya ya Waajiri Zanzibar (Zanema) kwa kuwa na ushirikiano mkubwa na serikali, hivyo kurahisisha ushughulikiaji wa changamoto mbalimbali zinazowakabili wafanyakazi.

"Nikupongezeni viongozi nyote wa shirikisho mnaomaliza muda wenu wa uongozi, hakika sote tunathamini kazi yenu kubwa na nzuri mliyoifanya katika kulitumikia shirikisho hili muhimu katika kipindi chote," alisema.

Akizungumzia kuhusu uchaguzi wa viongozi wakuu wa shirikisho hilo, Dk. Shein alisema ni haki kwa wajumbe wenye sifa kushiriki kwa uwazi pamoja na kuwachagua wagombea waliojitokeza baada ya kujiridhisha kuwa wana sifa na uwezo wa kuwatumikia wafanyakazi.

Naye, Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Moudline Castico, alisema serikali itaendelea kuwashughulikia kisheria waajiri wasiofuata sheria na miongozo ya serikali katika kuwapatia stahiki wafanyakazi wao.

Aliwataka wajumbe wanawake kujitokeza na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi wa shirikisho hilo ili kuendeleza mafanikio yaliofikiwa.

Katibu Mkuu wa ZATUC, Khamis Mwinyi Mohamed, aliipongeza serikali kwa kukubali uanzishaji wa sheria mbalimbali zinazohusiana na wafanyakazi nchini.

Aliipongeza serikali kwa kuviwezesha vyama vya wafanyakazi kufanya shughuli zake bila bughudha hatua yake ya kutoa nyongeza za mishahara kila baada ya kipindi, sambamba na mishahara hiyo kupatikana kwa wakati.

Alisema katika kipindi hicho (miaka mitano iliyopita), ZATUC kwa kushirikiana na serikali imekuwa na mchango mkubwa katika ukuaji na ustawi wa uchumi wa Zanzibar.

Vile vile, aliipongeza serikali kwa kuridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa pamoja na mikakati ya vipaumbele na kiufundi vya Shirika la Kazi Duniani (ILO).

## Kinamama wakumbusha jukumu la malezi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZAZI wametakiwa kutambua kuwa wataendelea kuwa na jukumu la kuzaa na kulea suala ambalo kwa wakati huu wengi wao hujisahau hasa katika ule mfumo wa asili wa malezi ya pamoja na badala yake kila mzazi huamua kulea mtoto wake pekee.

Mke wa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Asha Suleiman Iddi, aliyasema hayo wakati akilifungua Baraza la Wazazi la Chama Cha Mapinduzi la Wilaya ya Mfenesini linalofanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Mwalimu Nyerere uliopo Bububu, nje kidogo ya Mji wa Zanzibar.

Alisema hali ya ukosefu wa malezi ya pamoja kwa watoto imesababisha kuporomoka kwa maadili ya watoto wengi katika jamii na matokeo yake wanashindwa kuwaheshimu wazazi wa wenzao wakiona wa kwao ndio wanaostahiki kupata heshima hiyo.

Alisema watoto wa sasa wameacha maisha mazuri yanayoongozwa na utamaduni wa taifa na kuamua kufuata mila na tamaduni za ughaibuni jambo ambalo limechangia kuporomoka kwa maadili hasa wakiangaliwa watoto wenyewe, vizazi na mienendo yao tayari imeshapoteza hadhi ya utamaduni wa asili.

Alielezea masikitiko yake kutokana na vitendo vya udhalilishaji vilivyoshamiri katika mitaa mbalimbali nchini ambavyo kwa mtazamo wa matukio hayo, maadili tayari yameshapoteza mwelekeo kutokana na jamii ya sasa kukosea njia sahihi ya kuelekea.

Alisema tabia ya kupigwa kwa wanawake na watoto hadi kuumizwa na wakati mwengine kuchomwa moto watoto kwa makosa madogo pamoja na kutelekezwa ni miongoni mwa vyanzo vikuu vya udhalilishaji wa makundi hayo.

Alieleza kwamba ni ukweli usiofichika kwamba wanaoendeleza vitendo hivyo ambavyo ni vya kinyama na aibu kwa jamii yenye kufuata mila, silka, desturi na utamaduni wa watu wastaarabu ni wale waliokosa malezi ingawa wanaelewa fika ubaya wanaoufanya.

Vile vile, aliwataka wazazi na viongozi wa ngazi na nyanja zote pamoja na wananchi wote kuchukua tahadhari kwa kuwa karibu na familia zao ili kila mmoja kwa nafasi yake ailinde jamii kwa kukemea vitendo hivyo viovu vyenye kutia aibu.

Aliwataka viongozi wa jumuiya ya wazazi kuwa wana jukumu kubwa la kutoa elimu, kusimamia malezi bora ya watoto na kuhakikisha kwamba mazingira ya mitaa yanaimarika ipasavyo ili kuwa na jamii yenye ustawi na umakini mkubwa.

Akigusia janga la dawa za kulevya nchini ambalo huwakumba zaidi vijana wanaotarajiwa kuwa viongozi wa taifa la baadaye, alisema jamii bado inapaswa kukemea utumiaji wa dawa hizo ambazo ni janga linaloendelea kuikumba dunia na hatimaye kuathiri mataifa mengi ulimwenguni.

Akitoa taarifa fupi ya utekelezaji wa majukumu ya Jumuiya ya Wazazi Wilaya ya Mfenesini, Katibu wa Jumuiya hiyo, Biubwa Jabir, alisema yapo mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kazi za jumuiya hiyo ndani ya kipindi cha miezi sita iliyopita.

# Serikali yaahidi ushirikiano na kampuni mikopo nyumba

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKARI imesema kuwa itaendelea kushirikiana na Kampuni ya Mikopo ya Nyumba (TMRC) ambayo imeorodheshwa katika awamu ya pili katika hatifungani ya Soko la Hisa Dar es Salaam (DSE).

Hayo ameyasema Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Khatib Kazungu, katika hafla ya TMRC ya kuorodhoshwa katika hati fungani ya soko hilo iliofanyika jijini Dar es Salaam jana.

Alisema ni asilimia moja ya mikopo ya nyumba ikilinganishwa na nyingine, hivyo wadau lazima waongeze jitihada ya kutoka asilimia moja na kuongeza zaidi ili wananchi kupata mikopo nyumba zenye riba nafuu.

Alisema mpango wa ukopeshaji wa nyumba ulikuwa ukifanywa na Benki ya Nyumba Tanzania ambayo ilifilisika na serikali kukopa katika Benki ya Dunia na kuikopesha TMRC dola za Marekani milioni 70.

"Serikali itaendelea kushirikiana na wadau wote katika kukuza sekta ya nyumba nchini ikizingatiwa umuhimu wa umiliki wa nyumba," alisema Kazungu.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko na Dhamana na Mitaji (CMSA), Nicodemus Mkama, amesema mauzo ya toleo la kwanza yalikamilika Juni 8, mwaka jana ambapo TMRC ilifanikiwa kukusanya Sh. bilioni 12 ikiwa ni asilimia 4.3 ambayo ni zaidi ya lengo lililokuwa limetarajiwa.

Alisema toleo la pili la TMRC yamekuwa na mafanikio kwa Sh. bilioni 9.2 ikilinganishwa na Sh. bilioni nane zilizotarajiwa kukusanywa.

"Ongezeko hili linaonyesha imani walionayo wawekezaji wa Kampuni ya TMRC na CMSA na fedha zilizopatikana katika mauzo ya toleo la pili zitatumika kugharamia shughuli za maendeleo pamoja na kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa benki zinazotoa mikopo ya nyumba," alisema Mkama.

Alitoa wito kwa mifuko ya hifadhi ya jamii na taasisi za fedha kutumia njia ya masoko ya mitaji ili kuongeza ukwasi na uhakika zaidi.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Bodi ya TMRC, Theobald Sabi, alisema imeshatoa mikopo kwenye benki 15 yenye thamani ya Sh. bilioni 122.

TMRC iko katika mazungumzo na taasisi za kimataifa kwa ajili ya kupata mikopo nafuu ili mradi apate mikopo nafuu na riba.



Watoto wakicheza katika mazingira hatarishi pembezoni mwa nyumba zilizobomoka, eneo la Tandale, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## SMT, SMZ zajadiliana ushirikiano sekta kilimo

**Na Mwandishi Maalum**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Mhandisi Mathew Mtigumwe na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mansura Mosi Kassim, wameongoza kikao cha ushirikiano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania katika sekta ya kilimo.

Kikao hicho ni utekelezaji wa maagizo ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa wizara zote za SMT na SMZ kukutana na kuzungumzia ushirikiano kati yao.

Vikao kama hivyo hutuama kujadili kwa pamoja namna ya kutatua changamoto za Muungano zilizopo katika sekta ya kilimo.

Kikao hicho kulijadili utekelezaji wa maazimio mbalimbali yaliyowekwa katika kikao cha makatibu wakuu wa sekta ya kilimo kilichofanyika Machi, mwaka jana.

Kadhalika, maeneo mengine ya ushirikiano yaliyojadiliwa ni pamoja na maendeleo ya mazao, utafiti na mafunzo, huduma za umwagiliaji na zana za kilimo na sera, mipango na uimarishaji wa takwimu.

Kikao kazi hicho kilifanyika Juni 24, mwaka huu katika ofisi za Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Zanzibar.

ITV JARIDA LA WANAWAKE SAA 1:00 USIKU

LEO BLANDINA SEMBU ATAKUWA NA WANAKIKUNDI WA UMAKI KUTOKA JIJINI D`SALAAM WAKIZUNGUMZIA MAFUNZO KWA WANAWAKE NA WATOTO HASA KATIKA NIDHAMU, MILA, DESTURI NA PIA MAFUNZO YA MASUALA YA UPISHI WAKIITA JIKO LA AMANI.

# Wakulima wa pamba Mara wafurahia elimu ya vipimo

**Na Mwandishi Wetu,** MARA

WAKULIMA wa pamba mkoani Mara wameupongeza wakala wa vipimo nchini (WMA) kwa hatua yake ya kutoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya mizani inayotumika kwenye ununuzi wa zao hilo.

WMA imeendelea na uhakiki wa mizani zinazotumika katika vituo vya ununuzi wa pamba katika vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) ili kujiridhisha kama mizani hizo zinatumika kwa usahihi kwani baadhi ya wanunuzi wasiokuwa waaminifu huichezea na kuwaibia wakulima pamba.

Akizungumza na vyombo vya habari wilayani Musoma mkoani humo jana, mmoja wa wakulima hao, Peter Magesa alisema elimu ya vipimo imekuja wakati sahihi na itawafanya wawe makini kila wanapokwenda kuuza pamba.

"Elimu hii imetusaidia kujua mizani zimehakikiwa na Wakala wa Vipimo na kufungiwa lakiri (seal) pamoja na stika maalumu ya WMA.

"Pia tutahakikisha pointi zinazojitokeza wakati wa upimaji zinahesabiwa kwani awali wanunuzi wa pamba walikuwa hawahesabu pointi wakati wa upimaji na kudhulumu haki zetu.

"Na kwa upande wa kifungashio tutahakikisha tunakipima ili kujua uzito wake na kutoa uzito wa kifungashio katika furushi la pamba lililopimwa na siyo kukata kilo moja kwa kila kifungashio kwani vifungashio vinatofautiana uzito na havilingani," alisema mkulima huyo.

Meneja wa WMA, Jacob Lyambo, alisema kuwa kabla ya msimu wa pamba kuanza walishajiandaa vyema katika kuhakikisha haki ya mkulima haipotei kutokana na vipimo kutokuwa sahihi.

Alisema jumla ya mizani AMCOS 332 ilihakikiwa katika wilaya tano ambazo ni Serengeti, Musoma, Butiama, Bunda Mji pamoja na Bunda Vijijini.

Lyambo alisema katika uhakiki huo mizani minne ilikataliwa isitumike katika ununuzi wa pamba kutokana na kuwa na matatizo makubwa ambayo hayarekebishiki.

"Hivi sasa WMA Mkoa wa Mara inaendesha zoezi maalumu la uhakiki wa mizani zinazotumika kununulia pamba katika AMCOS mbalimbali kujiridhisha kama zinatumika kwa usahihi.

"Sambamba na hilo, elimu inatolewa kwa wakulima wa pamba juu ya utambuzi wa mizani sahihi na zilizohakikiwa na Wakala wa Vipimo, zoezi hili ni endelevu ambalo hufanyika kwa kushtukiza katika vituo hivyo ili kubaini wanunuzi wasio waadilifu wanaofanya vitendo vya uchakachuzi wa mizani,"alisisitiza meneja huyo.

Mpaka sasa AMCOS 78 zimeshapatiwa elimu na mizani zao kukaguliwa ambapo pia kwa mara ya kwanza mwaka huu Wilaya ya Rorya imeweza kulima pamba.

Elimu inayotolewa na WMA kwa wakulima ni pamoja na umakini pindi wanapokwenda kuuza pamba kwa kuhakikisha mizani inasoma sifuri (0) kabla ya kuanza upimaji kwa kutumia mizani ya digitali.

Baada ya kupima furushi la pamba mizani inatakiwa kurudi katika sifuri, na wahakikishe mizani haisomi hasi (-) baada ya kutoa mzigo na ikitokea imesoma hasi wamweleze karani anayesimamia mizani aweze kuizima na kuiwasha tena mizani hiyo kisha zoezi la upimaji liendelee.

# Nyadhifa za juu EU bado kitendawili

**LONDON,** Uingereza

NANI atarithi nafasi za juu katika Umoja wa Ulaya (EU) bado imekuwa fumbo licha ya wakuu wa jumuiya hiyo kujadiliana usiku kucha.

Viongozi hao bado hawajakubaliana kuhusu warithi wa Rais wa Baraza la EU, Donald Tusk na Rais wa Halmashauri ya EU, Jean Claude Juncker.

Hata baada ya kutumia muda wa saa 18 kujadiliana na viongozi hao wa EU bado hawajafikia makubaliano.

Maofisa wa EU wanasema viongozi wa EU wanakaribia kufikia makubaliano juu ya baadhi ya nafasi za juu na Frans Timmermans wa chama cha Leba cha nchini Uholanzi, anaonekana kuwa na nafasi nzuri ya kuchukua nafasi ya Jean-Claude Juncker kama rais mpya.

Hiyo ni kutokana na mkutano uliofanyika katika mkutano wa kilele wa viongozi wa nchi za G20 huko Japan wiki iliyopita.

Hata hivyo, pendekezo hilo limekutana na upinzani mkali kutoka nchi za Ulaya Mashariki pamoja na muungano wa vyama vya siasa za wastani za mrengo wa kulia EPP, hatua iliyomlazimisha Rais wa Baraza la Umoja wa Ulaya, Donald Tusk, kufanya mazungumzo kutafuta makubaliano ya kumuunga mkono mgombea mmoja.

Akizungumza na vyombo vya habari mjini Brussels, Tajani alisema mfumo wa Spitzenkandidat yaani mfumo unaozingatia kiongozi wa muungano aliyepata kura nyingi ndio unaofaa, kwa maana kwamba mgombea anayeongoza anapaswa kutoka kwenye kambi ya kisiasa iliyopata kura nyingi zaidi kwenye chaguzi za Ulaya.

Viongozi wa EU walieleza kuwa mkutano bado unaendelea lakini wanaelekea kuridhia wagombea watatu watakaochukua nafasi muhimu za usimamizi wa masuala ya mataifa 28 ya EU kwa miaka mitano ijayo.

Wagombea wanaotazamiwa kuchukua nafasi hizo za juu ni pamoja na Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje wa Uholanzi, Frans Timmermans ambaye anatazamiwa kuchukua wadhifa wa Rais wa Umoja wa Ulaya, Kristalina Georgieva wa Bulgaria huenda akamrithi Rais wa Baraza la Umoja wa Ulaya, Donald Tusk. **DW**

# Uturuki yampa onyo kali mbabe wa kivita Libya

**ANKARA,** Uturuki

UTURUKI imesema itafanya mashambulizi makali kwa vikosi vya kiongozi wa Libya, Jenerali Khalifa Haftar, endapo hawatawaachia huru haraka raia sita wa Uturuki.

Mwishoni mwa wiki vikosi vya Jenerali Haftar vilisema kuwa vitaishambulia Uturuki kwa kuwa taifa hilo linaunga mkono serikali ya Libya inayoungwa mkono na jumuiya ya kimataifa.

Vilevile walieleza kuwa waliharibu ndege isiyo na rubani ya Uturuki kwenye anga la Tripoli.

Libya imekumbwa na machafuko na mgawanyiko tangu kuondolewa madarakani na kuuawa kwa aliyekuwa kiongozi wa taifa hilo, Muammar Gaddafi mwaka 2011.

Jenerali Haftar alianza mashambulizi dhidi ya serikali inayotambuliwa na Jumuiya ya Kimataifa (GNA) inayoongozwa na Waziri Mkuu, Fayez al-Sarraj, Aprili, mwaka huu.

Uturuki inaunga mkono GNA, na kwamba imekuwa ikipeleka ndege zisizo na rubani, silaha na magari kwa ajili ya kusaidia juhudi za serikali kupambana na vikosi vya Jenerali Haftar, ambavyo vinadhibiti sehemu kubwa ya mashariki na kusini mwa Libya.

**Jenerali Haftar alirejea Libya wakati wa maandamano mwaka 2011 na kuwa kamanda muhimu wa kikosi cha mapinduzi Mashariki mwa Libya.**

Jenerali Haftar kutoka Jeshi la Taifa la Libya (LNA) alisema atashambulia meli za Uturuki zilizopo eneo la Libya na maeneo muhimu ya kibiashara ya Uturuki.

Pia, Jenerali Haftar amezuia ndege za kibiashara kutoka Libya kwenda Uturuki.

Juzi, Uturuki ilisema italipa kisasi kwa kuchukua hatua kali zaidi kwa vitisho vyovyote kutoka kwa vikosi vya Jenerali Haftar.

Waziri wa Ulinzi wa Uturuki, Huluski Akar alionya kuwa vikosi vya Libya vitalipa mashambulizi yoyote watakayofanya dhidi ya Uturuki. Uturuki ilieleza kuwa inataka kupunguza mapigano dhidi ya Jenerali Haftar, ambaye anaungwa mkono na Umoja wa Falme za Kiarabu na Misri.

Siku ya Alhamisi, GNA ilichukua mji muhimu wa Gharyan, ambao ni ngome ya vikosi vya Jenerali Haftar.

Kanali Muammar Gaddafi aliongoza Libya kwa miongo minne mpaka jeshi lilipomwondoa madarakani mwaka 2011. Tangu wakati huo, hakuna mamlaka iliyokuwa na udhibiti kamili wa nchi hiyo.

Khalifa Haftar jina lake limekuwapo kwa muda mrefu kwenye siasa za Libya kwa zaidi ya miongo minne na alikuwa mshirika wa karibu wa Gadaffi mpaka ulipotokea mgogoro mwaka 1980, ambao ulimlazimu kwenda kuishi uhamishoni nchini Marekani.

Jenerali Haftar alirejea Libya wakati wa maandamano mwaka 2011 na kuwa kamanda muhimu wa kikosi cha mapinduzi Mashariki mwa Libya.

Vikosi vya Jenerali Haftar vinaungwa mkono na Ufaransa, Misri na Umoja wa Falme za Kiarabu.

Aprili, mwaka huu Rais wa Marekani, Donald Trump, alionekana kumuunga mkono. **BBC**



Raia wa Sudan wakiwa katika maandamano wakidai wanajeshi kukabidhi madaraka ya nchi kwa wananchi. **PICHA: REUTERS**

# Saba wauawa wakati wa maandamano Sudan

**KHARTOUM,** Sudan

WATU saba wameuawa wakati wa mapigano makali yakitokea kati ya wanajeshi na waandamanaji nchini Sudan.

Hali ya usalama imeendelea kuwa tete nchini Sudan, huku jeshi likiendelea kushinikizwa kukabidhi madaraka kwa raia. Watu zaidi ya 200 wamejeruhiwa katika makabiliano hayo.

Maelfu ya wananchi Sudan waliandamana wakilitaka jeshi kukabidhi madaraka kwa raia.

Katika Mji Mkuu wa Khartoum, umati wa waandamanaji waliweza kufika kwenye Ikulu ya Rais, ambayo ni makao makuu ya Baraza la Jeshi la Mpito (TMC).

Hata hivyo, jeshi lilitumia mabomu ya machozi kwa kuwatawanya waandamanaji.

Mamia ya askari wa akiba kutoka Kikosi cha Usaidizi wa Haraka (FSR) walitumwa katika maeneo mbalimbali ya Mji Mkuu Khartoum.

"Ujumbe wa askari hao ilikuwa kulinda waandamanaji, lakini hatukuamini watu walioshirikiana na waandamanaji, kulikuwapo na watu kadhaa wenye silaha ambao waliwafyatulia risasi askari watatu wa Kikosi cha Usaidi wa Haraka (FSR)," alisema Makamu wa Rais wa Baraza la Jeshi la Mpito (TMC), Mohamed Hamdane Daglo.

Hali hiyo imetokea wakati Jumuiya ya Kimataifa ikitoa wito kwa jeshi kuacha kutumia nguvu kubwa dhidi ya waandamanaji kama ilivyotokea mwanzoni mwa mwezi.

Viongozi wa waandamanaji walikuwa wameitisha maandamano ya watu milioni moja, lakini kwa sababu ya kukamatwa kwa huduma ya mtandao, imekuwa ni vigumu waandamanaji kukusanyika kama hapo awali.

Licha ya waandamanaji kupiga kambi katika Wilaya ya Bari na Mamura na Arkweit, Mashariki mwa Jiji la Khartoum, walifukuzwa na maofisa wa polisi.

Maandamano hayo yamefanyika wakati huu Umoja wa Afrika (AU) na Ethiopia kwa pamoja zikiwasilisha mikataba ya kuunda serikali ya mpito kati ya wanajeshi na waandamanaji. **RFI**

# Wasomi wachapisha kazi majarida feki

Na Salome Kitomari

RAIS wa Akademia ya Sayansi, Prof. Yunus Mgaya, amesema watafiti wengi nchini wameingia kwenye mkumbo wa kuchapisha kazi zao kwenye majarida ya kitapeli ambayo hayana hadhi ya kimataifa.

Prof. Mgaya aliyasema hayo mbele ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, wakati wa uzinduzi wa baraza jipya la taasisi ya wasomi isiyo ya kiserikali ijulikanayo kama Akademia ya Sayansi.

Alisema watafiti wengi wamejikuta kwenye mikono ya mapateli wa nchi za Afrika Magharibi kwa kudanganywa kuwa kazi zao zitachapishwa kwenye majarida makubwa duniani, lakini wanapofuatilia wanakuta ni utapeli na kazi zao hazimo kwenye majarida ya kimataifa.

Kutokana na hali hiyo, Prof. Mgaya alisema katika mpango mkakati wao, Akademia imepanga kuwaunga mkono wanasayansi kuchapisha kazi zao za kitafiti katika majarida ya kitaifa yenye hadhi ya kimataifa.

Prof. Mgaya alitaja mipango mkakati mingine ni kuongeza idadi ya wanachama na kuimarisha ushiriki wao katika shughuli za Akademia, uwezo endelevu wa kifedha, kiutawala, rasilimali watu na miundombinu, kuimarisha mitandao na ushirikiano kwenye masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

Nyingine ni kuongeza ubora wa sayansi, teknolojia na ubunifu kitaifa, kuifanya sayansi, teknolojia na ubunifu kuwa sehemu ya sekta za kijamii-kiuchumi na umma wa wote kwa ujumla, kuimarisha upatikanaji wa ushauri wa kisayansi, kiteknolojia na ubunifu kwa serikali, wanasiasa na taasisi za kikanda na kimataifa.

Nyingine kuimarisha uzalishaji, uhifadhi na usambazaji wa maarifa asilia na yale tunayojifunza darasani kuhusiana na sayansi, teknolojia na ubunifu.

Aidha, Waziri Ndalichako alisema kuporomoka kwa nafasi ya vyuo vikuu nchini vinavyofanya vizuri Afrika kunatokana na watafiti wengi kufanya kazi na kuzifungia makabatini badala ya kuzichapisha kwenye majarida ya kimataifa.

"Vyuo vyetu kitaaluma viko vizuri sana lakini kwenye uchapishaji wa kazi za kitaaluma ndiyo hatufanyi vizuri. Katika kuangalia vyuo bora moja ya mambo yanayoangaliwa ni idadi ya kazi zilizochapishwa kwenye majarida ya kimataifa, lakini za kwetu nyingi zinaishia kwenye makabati," alisema.

Waziri Ndalichako alisema wizara imechukua hatua za kuhamasisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika shughuli za maendeleo ya jamii.

Awali, Rais mstaafu wa Baraza la Akademia, Prof. Esther Mwaikambo, aliiomba serikali kutunga sheria itakayoitambua taasisi hiyo kama zilizvyo nyingine za aina hiyo za nchi nyingine zinazotambulika kimataifa.

Alisema Akademia imeendeleza na kukuza mikakati ya kujiunga kwenye mitandao na kushirikiana na jumuiya nyingine za kisayansi kama njia ya kubadilishana uzoefu, rasilimali na maarifa na kuendeleza matumizi ya utafiti wa kisayansi katika kushauri serikali na wadau wengine.



Kaimu Mkurugenzi wa Masoko na Huduma kwa Wateja wa Shirika la Bima la Taifa (NIC), Elisante Maleko (kulia), akimkabidhi nyaraka Daisy Doris John mkazi wa Mbagala jijini Dar es Salaam baada ya kujiunga na Bima ya Elimu inayotolewa na NIC. Wa pili kushoto ni Catherine Mashimba Ofisa Bima wa NIC na wa tatu kushoto ni Ofisa wa Bima, Vincent Rogath. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shahidi ataja damu kesi ya Mbowe

INATOKA UK 8

**Kibatala:** Uliwahi kutoa maagizo kuhusu kuongezewa damu Konstebo Fikiri?

**Shahidi:** Hapana.

**Kibatala:** Nani alimshona Konstebo Fikiri?

**Shahidi:** Mimi hapa na niliagiza ahudhurie kliniki kwa mtaalamu wa upasuaji.

Kesi hiyo inaendelea leo kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri.

Jopo la utetezi liliongozwa na Wakili Profesa Abdallah Safari, Peter Kibatala, John Mallya na Hekima Mwasipu.

Mbali na Mbowe, washtakiwa wengine ni Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya; Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko; Katibu Mkuu wa Chadema, Vicent Mashinji; Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika; Mbunge wa Kawe, Halima Mdee na Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Februari Mosi na Februari 16, mwaka huu Mbowe na wenzake wakiwa Kinondoni, Dar es Salaam kwa pamoja walikula njama na wengine ambao hawapo mahakamani ya kutenda kosa la jinai ikiwamo kuendelea na mkusanyiko isivyo halali na kusababisha chuki na uchochezi wa uasi.

Ilidaiwa kuwa Februari 16, mwaka jana, Bulaya alishawishi kutenda kosa la jinai katika viwanja vya Buibui vilivyoko Kinondoni, Dar es Salaam kwa kuwataka wakazi wa eneo hilo kufanya maandamano yenye vurugu.

Pia ilidaiwa kuwa Februari 16, mwaka jana katika barabara ya Kawawa eneo la Konondoni Mkwajuni kwa pamoja washtakiwa na wenzao zaidi ya 12, walifanya mkusanyiko na kukaidi amri halali ya ofisa wa Jeshi la Polisi Gerald Ngiichi na kusababisha kifo cha Akwilina Akwiline na askari polisi wawili Konstebo Fikiri na Koplo Rahim Msangi kujeruhiwa.

Ilidaiwa siku ya tukio la kwanza na la pili, katika viwanja vya Buibui, kwenye mkutano wa hadhara, Heche alitoa lugha ya kuchochea chuki alitamka matamshi kwamba: "Kesho patachimbika upumbavu ambao unafanywa kwenye nchi hii...wizi unaofanywa na serikali ya awamu ya tano... watu wanapotea... watu wanauawa wanaokotwa kwenye mitaro lazima ukome... "ambayo yanadaiwa yalielekea kuleta chuki kati ya serikali na Watanzania.

## Hasunga, bosi Usaid wateta Dar

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, jana alikutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (Usaid), Andy Karas, katika ofisi za wizara jijini Dar es Salaam.

Katika mazungumzo hayo, Hasunga alimweleza mkurugenzi huyo kuwa wizara imejipanga kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya kilimo, ili kuondokana na dhana ya kilimo cha kujikimu na kuhamia katika kilimo cha kibiashara.

Waziri Hasunga alisema ili kuongeza tija katika sekta hiyo, wizara imejipanga kuimarisha utafiti.

Alisema maendeleo ya kilimo yanategemea zaidi utafiti hususani wa udongo na pia kubaini teknolojia bora itakayosababisha kukisogeza kilimo katika hatua kubwa ya mafanikio na kimageuzi.

Alisema pamoja na mambo mengine, wizara pia imejipanga katika kuongeza thamani ya mazao ya kilimo kuliko kusafirisha yakiwa ghafi au hayajaongezewa thamani.

"Tukiongeza thamani ni wazi kuwa uchumi utapanda, lakini zaidi ajira zitaongezeka kwa wananchi. Tutakuwa na pato zuri la kigeni sambamba na utambulisho wa nchi," alisema Hasunga.

Kuhusu sekta ya umwagiliaji, Hasunga alisema Tanzania ina zaidi ya hekta milioni 29 zinazofaa katika umwagiliaji lakini ni hekta 475,000 ndizo ambazo zimefanyiwa kazi.

"Kwa maana hiyo kuna fursa kubwa katika umwagiliaji, hivyo natoa wito kwa wadau wengine kujitokeza kuwekeza katika umwagiliaji," alisema.

Kuhusu lishe, Waziri Hasunga alisema wizara imeendelea kuweka hamasa kwa wakulima ili kuwa na lishe bora. Aliongeza kuwa Watanzania wanapaswa kuwa na utamaduni wa kula vizuri ili kuondokana na magonjwa mbalimbali kama vile utapiamlo.

Naye Karas aliipongeza serikali ya awamu ya tano kwa mikakati madhubuti ya kuimarisha sekta ya kilimo nchini.

Aidha, Karas alimwomba Waziri Hasunga kuteua watu wawili kutoka wizarani watakaokuwa kiungo muhimu baina ya serikali na miradi ya Usaid sambamba na mtu atakayeratibu mikutano ya wadau wa maendeleo.

## Samia kufungua maonyesho Sabasaba

INATOKA UK 7

"Ningependa wawekezaji wa ndani na waliowekeza kutoka nje ya nchi kuyatumia maonyesho haya kama jukwaa la fursa ya kuwakutanisha na dunia kwa ajili ya kunadi wanavyozalisha," alisema.

Alisema Sabasaba ya mwaka huu imekuwa na mwamko mkubwa kwa sababu hata nchi shiriki zimeongezeka kutoka 33 mwaka jana hadi 35 huku kampuni za ndani zikiongezeka pia kutoka 2956 mwaka jana, wakati sasa ni 3250.

Aliongeza lengo kuu ni kuwainua wakulima na wafanyabiashara wadogo kupitia biashara zao, huku akisisitiza wakulima kujikita katika kilimo cha kimkakati.

"Tunafungamanisha kilimo na Viwanda kwa sababu kilimo kinajumuisha mambo mengi ikiwamo ufugaji... Wizara haiangalii kampuni kubwa pekee bali inaangalia na viwanda vidogo ili kujua kuwa mikakati yao inabadilisha maisha ya Watanzania," alisema.

Alisema pia bado kuna viwanda ambavyo vinalalamika kutokuwapo kwa nguvukazi ilhali vijana wanalalamika uchache wa ajira nchini.

Bashugwa aliongeza kuwa ameiagiza SIDO kutoa mafunzo yanayohitajika kwa vijana ili kuwa na watakaokuwa na uwezo wa kufanya kazi hiyo.

## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

### NAFASI ZA KAZI


**TANGAZO LA KAZI,** Wanahitajika IT – Diploma, Sales Lady, Messenger – awe mvulana. Elimu kidato cha nne/ cha sita. Wawe wazoefu wa kutosha. Mawasiliano: 0715 885533. Email: jmtofficetraders96@gmail.com au jmtofficetraders@gmail.com.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**


### VYETI VIMEPOTEA



**JENIPHER J. MINJA** anatangaza kupotelewa na **Cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0329/0013** kilichotolewa na MAKUMIRA SEKONDARI mwaka 2003. Cheti cha Ualimu chenye index namba **E513/0112** kilichotolewa na CHUO CHA UALIMU MANDAKA mwaka 2008. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MKU/RB/2468/2019.**

115303702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI KWA MDAIWA**

**MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU WILAYA YA GEITA**

**SHAURI LA MADAI NAMBA 31/2019**

**MDAI: HAPPINESS KASSIM**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: STEPHANO KITULA WA MWANZA.**

**AMRI**

**UNAAMRIWA NA MAHAKAMA UHUDHURIE HAPA MAHAKAMANI MNAMO TAREHE 10.7.2019 SAA 2.30 ASUBUHI BILA KUKOSA.**

USIPO HUDHURIA SHAURI HILI LINAWEZA KUSIKILIZWA UPANDE MMOJA BILA YA WEWE KUWEPO NA KUTOLEWA UAMUZI.

HATI HII IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA MHURI WA MAHAKAMA LEO TAREHE 20. 6. 2019.

115303902

---

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**TANZANIA CHINA TRADE & TOURISM DEVELOPMENT LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya PIKIPIKI aina **HAOJUE** yenye namba za usajili MC805BSE . Chassis namba **LC6PCJK27HOO17895.** Engine No. **156FMI5AD2F22617.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/TR/RB/2618/2019**

115304002

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA –MWANZA**

**SHAURI NA 395 LA 2018**

**ELIBARIKI JACKSON NSHIU........................................... MDAI**

1. **NATIONAL MICROFINANCE BANK**
2. **NSOMBO& COMPANY LIMITED**
3. **JOEL CHARLES FOYA**
4. **GERMA GILIARD MAEDA....................................WADAIWA**

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

**KWA: JOEL CHARLES FOYA NA GERMA CILIARD MAEDA**

Mnafahamishwa kwamba mjibu maombi hapo juu amefungua shauri/ ombi dhidi yenu katika baraza la Ardhi na nyumba mkoa wa Mwanza ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 23/07/ 2019 katika chumba cha baraza barabara ya posta jengo liko mkabala na mahakama kuu ya Tanzania.

kwa hivyo mnatakiwa kuhudhuria katika baraza siku hiyo nyinyi wenyewe, wakili wenu au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria kujibu ombi hilo na kutoa uamuzi bila nyinyi kuwepo.

Imetolewa nami kwa Amri na chapa ya Baraza leo tarehe 13/06/2019

115304102

---

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOHN V. MSHANGA ANATANGAZA** KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 934 CPL** AINA YA SUZUKI CAARY RANGI NYEUPE. CHASSIS NAMBA **DB52T130704.** ENGINE NAMBA F6A6915419. YEYOTE ATAKAYEIONA ATAOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI: **OB/RB/2334/2019.**

115304702


# JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

## NI JIBU LAKO

## NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

## KWA BEI NAFUU SANA

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# RABIOT AJIFUNGA MITANO JUVENTUS




**TURIN,** Italia

KIUNGO Adrien Rabiot, amewasili nchini Italia kwa ajili ya kusaini mkataba wa miaka mitano kujiunga na Klabu ya Juventus.

Mkataba wa Rabiot pale Paris Saint-Germain ulimalizaka Juni 30, mwaka huu baada ya pande hizo mbili kushindwa kufikia makubaliano ya kuongeza mkataba mpya.

Kiungo huyo hakuchezeshwa mechi hata moja kwenye kipindi cha pili cha msimu wa 2018/19, huku Kocha wa PSG, Thomas Tuchel akimuweka benchi.

Hivi karibuni iliripotiwa kwamba, Juventus na Rabiot walifikia makubaliano binafsi kwa maslahi yake na sasa ametua kusaini mkataba.

Juventus iliposti video kwenye mtandao wake wa kijamii wa twitter kuthibitisha kwamba Rabiot yupo nchini Italia kukamilisa usajili huo, akionekana akitua mjini Turin.

Juventus pia waliandika kwenye twitter yao mapema juzi asubuhi kwamba habari nzuri zinakuja kuanzia jana Julai Mosi.

Goal.com imeripoti kwamba Rabiot jana Jumatatu alifanyiwa vipimo vya afya, kabla ya kutia saini mkataba wa miaka mitano na 'Bianconeri' hao.

Dili hilo litamfanya Rabiot kuingiza kitita cha pauni milioni sita kwa msimu na mama yake Veronique, ambaye ndiye wakala wake, atatia mfukoni pauni milioni tisa kama ada yake kwa ajili ya usajili wa mchezaji huyo.

## *Suarez wa Barca auzwa Celta Vigo*

**BARCELONA,** Hispania

CELTA Vigo imetangaza kumnasa kiungo wa Barcelona, Denis Suarez, ambaye anajiunga na vigogo hao wa La Liga kwa euro milioni 12.9, pamoja na ongezeko la euro milioni 3.1.

Suarez alitumia nusu ya kipindi cha pili cha msimu wa 2018/19 akicheza kwa mkopo pale Arsenal baada ya kukosa namba kule Barcelona, lakini kiungo huyo alishindwa kuonyesha kiwango chake kwa miamba hao wa London kaskazini na hakupenya katika kikosi cha kwanza cha kocha, Unai Emery.

Barcelona imethibitisha kuondoka kwa Suarez katika taarifa yake iliyowekwa kwenye tovuti yao, ambayo inasomeka: "FC Barcelona na Celta Vigo wamefikia makubaliano ya uhamisho wa mchezaji Denis Suarez. Celta Vigo watailipa Barcelona euro milioni 12.9 pamoja na nyongeza ya euro milioni 3.1.

"FC Barcelona inapenda kumshukuru Denis Suárez kwa kipindi chake alichokuwa na sisi na tunamtakia mafanikio mema huko anakokwenda."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, alianza kucheza soka la ushindani akiwa Celta Vigo, akiwa amekulia kwenye academi kabla ya kujiunga na Manchester City na baadaye Barcelona.

Kuondoka kwa Suarez pale Barcelona ni wakati mzuri zaidi kwake kuweza kupata nafasi nyingine ya kucheza, kwani yeye mwenyewe alibainisha kwamba kipindi cha majira ya joto angependa kuondoka.

"Nataka kuondoka Barca na kupata nafasi ya kucheza sehemu nyingine," alisema katika mahojiano na redio Catalunya mwanzoni mwa msimu huu. Aliongeza; "Lakini nataka kubaki kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga."



## Mmiliki Liverpool ataka ubingwa EPL



**LIVERPOOL,** England

MMILIKI wa Klabu ya Liverpool, John Henry amesema klabu yake imejipanga kuhakikisha inatwaa taji la Ligi Kuu ya England msimu ujao, baada ya kulibeba lile la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Liverpool haijashinda taji la Ligi Kuu ya England tangu mwaka 1990 na licha ya kumaliza ikiwa na pointi 97 msimu uliopita, ilipitwa kwa pointi moja na Manchester City walioutwaa ubingwa huo.

Na sasa Henry amesema malengo yake ni kumaliza ukame wa miaka 30 wa kutolibeba taji hilo na wamejipanga kuhakikisha wanalitwaa msimu ujao.

"Kwangu mimi taji la Ulaya ni kubwa kuliko la Ligi Kuu England, lakini nafikiri ni kweli kwamba mashabiki wanalitaka hilo sasa," alisema Henry akinukuliwa na Gazeti la Daily Mail.

"Najua akili yetu itajikita kuhakikisha tunashinda taji la Ligi Kuu msimu ujao na hayo ndio malengo yetu."

Henry, yupo nchini England ambako alikwenda kushuhudia mchezo wa Boston Red Sox dhidi ya New York Yankees wa Ligi Kuu ya mpira wa magongo ya Marekani ambao ulichezwa pale West Ham.

# Inter Milan yabomoa safu ya ulinzi Atletico Madrid

**MILAN,** Italia

INTER Milan imemsajili Diego Godin kwa uhamisho huru baada ya nahodha huyo wa Uruguay kuondoka Atletico Madrid mwishoni mwa msimu uliopita.

Mwezi uliopita mtandao wa ESPN FC uliripoti kwamba, Godin amesaini mkataba wa miaka mitatu wenye thamani ya euro milioni 6.75 pale kwenye dimba la San Siro, na Nerazzurri hao wamethibitisha jana Julai Mosi, siku ambayo dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto nchini Italia lilifunguliwa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, amekuwa mchezaji mpya kusainishwa na kocha wa Inter, Antonio Conte tangu alipoteuliwa kuwa kocha akichukua nafasi ya Luciano Spalletti.

Godin aliwaita waandishi wa habari kutangaza kwamba anaondoka Atletico mwishoni mwa msimu huu, mkutano ambao ulihudhuriwa na wachezaji wenzake wote pamoja na kocha Diego Simeone, lakini hakuweka wazi wapi anakwenda.

Baada ya kumalizika kwa msimu wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, alijiunga na kikosi cha Uruguay kwenye michuano ya Copa America, ambapo La Celeste walitolewa hatua ya robo fainali na Peru kwa mikwaju ya penalti.

Inter ilifuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya siku ya mwisho ya kumalizika msimu, lakini walimaliza wakiwa wamepitwa pointi 21 na vinara Juventus kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Conte pia anatafuta mshambuliaji mpya wa kati kipindi hiki, huku nyota wa Manchester United, Romelu Lukaku akitajwa kuwa ndiye chaguo lake namba moja.






# RASHFORD AOGELEA NOTI MAN UNITED

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United ipo tayari kumfanya Marcus Rashford kuwa mmoja wa wachezaji wake anayelipwa kitita kikubwa zaidi cha fedha, baada ya kufikia muafaka wa mazungumzo yao ya kusaini mkataba mpya, ESPN FC imedokeza.

Rashford anakaribia kusaini mkataba wa miaka mitano wa kuendelea kukaa hapo kwenye dimba la Old Trafford huku mshahara wake ukitajwa kupanda zaidi.

Chanzo kimoja ndani ya Man United kimeiambia ESPN FC kwamba, mshahara mpya wa Rashford hautakuwa sawa na ule anaolipwa Alexis Sanchez wa pauni 391,000 kwa wiki, lakini atafikia kiasi cha kulipwa pauni 200,000 kwa wiki.

United inajua kwamba, mshambuliaji huyo wa kimataifa wa England amekuwa akiwaniwa na klabu kama Barcelona, Real Madrid na Manchester City, lakini sasa wana imani watambakisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21.

'Dogo' huyo aliyekulia kwenye academi ya klabu hiyo tangu akiwa na umri wa miaka saba, Rashford ndiye tegemeo la kocha Ole Gunnar Solskjaer kama mshambuliaji wake wa kati.

Nyota mwingine aliyekulia kwenye academi hiyo, Jesse Lingard, anakaribia kusaini mkataba mpya, ingawa mazungumzo rasmi bado hayajaanza.

Rashford alichomoza chini ya zama za kocha, Louis van Gaal mwaka 2016 na amefunga mabao 45 katika mechi 170 tangu alipoanza kuichezea timu ya wakubwa Februari mwaka huo, pia akicheza mechi 32 kwa timu ya Taifa ya England.

# Ndombele atua kwa rekodi Spurs

**LONDON,** England

TOTTENHAM Hotspurs imekubali kulipa kiasi cha euro milioni 62 kwa Klabu ya Lyon ambayo inaweza kupanda hadi euro milioni 72 kwa ajili ya usajili wa mchezaji, Tanguy Ndombele, ESPN FC imeripoti.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 22, atakua mchezaji aliyeweka rekodi ya usajili kwa klabu hiyo ya Ligi Kuu England, akiipiku ile ya pauni milioni 42 waliyolipa kule Ajax kwa kumsainisha mkataba Davidson Sanchez mwaka 2017.

Maslahi binafsi bado hayajafikiwa, lakini hilo si tatizo na usajili wake unatarajiwa kutangazwa mapema wiki hii.

Mchezaji huyo anapanga kusafiri kwenda jijini London kwa ajili ya kufanyiwa vipimo vya afya ili kuwa tayari kujiunga na wachezaji wenzake Julai 8, mwaka huu.

Ilikuwa muhimu kwa pande zote mbili, Ndombele na kocha Mauricio Pochettino kwamba kiungo huyo kuwa sehemu ya klabu katika maandalizi ya msimu mpya wa ligi.

Baada ya wiki kadhaa ya makubaliano, huku akisafiri kwenda kwenye uwanja mpya wa Spurs na katika kituo cha mazoezi na kuzungumza mara kadhaa na Pochettino, hatimaye Ndombele akakubali kutua hapo.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ASENSIO SASA CHAMBO YA MANE KUTUA REAL

●●● Tunaahidi kupigania kuongeza nguvu katika kila kombe hadi mwisho, Madrid mara zote...

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid inajaribu kuishawishi Liverpool kuiachia mshambuliaji wa kimataifa wa Senegal, Sadio Mane majira haya ya joto huku ikiwa tayari kuipa fedha pamoja na Marco Asensio, taarifa zimeeleza.

**Gazeti la 'The Sunday Express' linaamini kuwa kocha mpya wa Real Madrid, Mfaransa Zinedine Zidane anatumai kumuongeza Mane katika kikosi chake kipya, huku akimwachia Asensio.**

Zidane ni wazi amejiandaa kumruhusu kiungo huyo Mhispania kuondoka Bernabeu wakati huu taarifa zikidai kuwa Jurgen Klopp ni shabiki wa Asensio.

Kuwika kwa Mane kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kumemuweka sawa Zidane, ambaye anataka kumuongeza katika safu yake mpya ya ushambuliaji ambayo tayari ina Eden Hazard, Luka Jovic na Rodrygo, lakini Klopp hatakubali kubaribisha pendekezo kama hili - kama ni kweli.

Mapema mwezi huu AS lilidai kuwa miamba hiyo ya La Liga imepanga takriban dau la pauni milioni 80 hadi 88 kwa Asensio na Liverpool, Spurs pamoja na Manchester United zote zinafahamika kuvutiwa na kiungo huyo.

Aidha, ESPN hivi karibuni ilieleza kuwa Klopp anaweza kurejea katika lengo lake la kuipata huduma ya nyota huyo wa kimataifa wa Hispania, ambaye anaweza kufurahi kwa kupata nafasi ya kucheza chini ya Mjerumani huyo ili kumsaidi kufikisha kiwango chake katika daraja la juu.

Ingawa Mei, Asensio alitupia katika ukurasa wake wa Instagram akieleza hana lengo la kuondoka Bernabeu majira haya ya joto, na taarifa ya hivi karibu kupitia Gazeti la Express ina mambo kidogo ya kutushawishi kwamba anaweza kwenda England majira haya ya joto.

"Msimu wa utata, ambao umekuwa mgumu kabisa, Umekamilisha. Ilikuwa mbali na kiwango ambacho mashabiki wetu wa ajabu wanastahili," Mhispania huyo alisema.

"Tutachagua wenyewe kuwa juu, tutakuwa bora na tutajitoa kwa kila kitu, hivyo mashabiki wa Madrid watakuwa tayari kufurahia timu yao tena msimu ujao [tunapoangalia] kurudia msaada wako usio na masharti na upendo.

"Tunaahidi kupigania kuongeza nguvu katika kila kombe hadi mwisho."Madrid mara zote inatokea nyuma. Hala Madrid!"

## ZISIKUPITE

### LIVER KUMREJESHA COUTINHO

LIVERPOOL imefungua milango ya kumrejesha Mbrazil Philippe Coutinho, 27, klabuni hapo baada ya kiungo huyo kupata wakati mgumu Barcelona. ***(Le10 Sport, via Mirror)***

### SPURS KUMKOSA NDOMBELE

MANCHESTER United bado inaweza kuipiku Tottenham katika mbio za kuipata saini ya kiungo wa Lyon, Tanguy Ndombele, 22, ambayo imekubaliana ada na klabu hiyo ya Ligue 1, lakini ikiwa bado haijakamilisha malipo binafsi na nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa. ***(L'Equipe, via Metro)***

### KUMUUZA MATUIDI, KHEDIRA

JUVENTUS inajiandaa kumuuza nyota wa kimataifa wa Ufaransa, Blaise Matuidi na kiungo mwenzake, Mjerumani Sami Khedira, wote kila mmoja akiwa na miaka 32. ***(Tuttosport, via Calciomercato)***

### NAPOLI YAIFUATA ARSENAL

NAPOLI inapanga kumfuata beki wa Celtic, Kieran Tierney, wakati huu Arsenal ikiwa bado haijatoa ofa inayokubalika kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Metro)***

### AHOFU UBORA WA NEYMAR

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amesema hana uhakika "kama Neymar atakuwa na ubora ule ule" akirudi Barcelona akitokea Paris St-Germain kama ilivyokuwa kipindi chake cha kwanza wakati nyota huyo wa kimataifa wa Brazil akiwa klabuni hapo. ***(Ara, via Mirror)***

### LUKAKU HAMZUII BEN YEDDER

MANCHESTER United imekubaliana malipo binafsi na mshambuliaji wa Sevilla, Wissam 28, na nyota huyo wa Ufaransa anaweza kutua Old Trafford bila kujali kama watamuuza Mbelgiji Romelu Lukaku, 26. ***(Express)***

### FERNANDES BADO LULU UNITED

KIUNGO mshambuliaji wa Ureno, Bruno Fernandes, 24, bado anaweza kuondoka Sporting Lisbon na kujiunga na Manchester United, wakati huu klabu hiyo ya Ligi Kuu England ikijiandaa kupiga hatua katika nia yao hiyo. ***(Manchester Evening News)***

### IZZO NGUMU ARSENAL, EVERTON

ARSENAL na Everton zinamuwinda Armando Izzo, na hataondoka Torino, kufuatia klabu hiyo ya Serie A kutokuwa tayari kumuuza beki huyo. ***(Calciomercato)***

### LAMPARD KURITHIWA DERBY

DERBY County inamtaka nyota wa zamani wa kimataifa wa Uholanzi, Phillip Cocu kuwa mbadala wa kocha Frank Lampard, ambaye anatarajiwa kwenda kuinoa Chelsea. ***(Times)***

### SPURS KUMBAKISHA CLARKE

TOTTENHAM itamtoa kwa mkopo kiungo Jack Clarke, kwa Leeds United baada ya kumsajili nyota huyo aliyekuwa akiichezea miamba hiyo ya Elland Road. ***(Guardian)***

### JUVE YAMGEUKIA MCNEIL

JUVENTUS inapanga kutoa ofa kwa winga wa Burnley na England U-20, Dwight McNeil, 19. ***(Sun)***

HABARI MICHEZO

## Uganda yapania kutoboa 16-bora

**Na Mwandishi Wetu,** CAIRO

LICHA ya kupoteza mchezo dhidi ya wenyeji Misri, Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Uganda (The Cranes), Sebastien Desabre, amesema anaamini kikosi chake kina nafasi ya kufanya vema katika mechi ya hatua ya 16-bora kutokana na uwezo ambao wachezaji wake wanao.

Uganda ilifungwa mabao 2-0 na Misri na kuwafanya wababe hao kutoka Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), kumaliza hatua hiyo ya makundi wakiwa na pointi nne, nyuma ya vinara wenyeji hao wenye pointi tisa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wenye pointi tatu wakiwa watatu na Zimbabwe yenye alama moja ikiburuza mkia kwenye Kundi A. Desabre alisema kuwa bado wako katika mapambano na wanaamini wataendelea kupeperusha vema bendera ya Uganda katika fainali hizo za Kombe la Mataifa Afrika zinazotarajiwa kumalizika ifikapo Julai 19, mwaka huu.

Mfaransa huyo alisema mechi zote ni ngumu, na kila mchezaji anayepata nafasi ya kucheza, anaonyesha uwezo wake kwa sababu walikuja Misri kupambana na si kusindikiza wengine.

"Ulikuwa mchezo mgumu sana, hasa unapocheza na mwenyeji, mbali na kiwango cha timu yake, kuwa nyumbani huongeza morali kwa wachezaji, kila timu ilihitaji kushinda ili kujiweka katika nafasi nzuri zaidi kwenye kundi, ila tunaahidi tutakuwa na ari ya juu zaidi katika mchezo wetu unaokuja," alisema Desabre.

Kocha Mkuu wa Misri, Javier Aguire, alisema kuwa kila mechi kwao ni sawa na fainali na hivyo wanacheza kwa umakini na tahadhari kuhakikisha malengo yao yanatimia.

Naye Kocha Mkuu wa Zimbabwe, Sunday Chidzambwa, aliliambia gazeti hili kuwa kikosi chake hakikuwa na bahati ya kupata ushindi katika fainali hizi.

"Tulicheza vizuri, lakini tulishindwa kutumia nafasi tulizopata, tunarudi nyumbani kusahihisha makosa yetu, kwa mwaka huu, hatukuwa na nafasi ya kupata hata pointi moja, tutatumia mashindano haya kujiandaa na michuano mingine," Chidzambwa alisema.

Mbali na Zimbabwe, timu nyingine ambazo zimeyaaga mashindano hayo ni Burundi na Taifa Stars ambayo jana usiku ilikuwa inamalizia mchezo wake wa mwisho dhidi ya Algeria.

# MO AIMWAGIA SIMBA MIL. 250/-

**Na Shufaa Lyimo**

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wenye makao yake makuu Msimbazi jijini Dar es Salaam, wameingia mkataba wa mwaka moja wenye thamani ya milioni 250/- kupitia kinywaji cha Mo Xtra chini ya Kampuni ya A One ya Mohammed Enterprises.

Akizungunza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugezi wa Masoko wa METL, Fatma Dewji alisema udhamini huo ni muendelezo wa ule walioingia mwaka jana kupitia kinywaji cha Mo Energy.

Alisema Mwaka huu wanaendelea na udhamini huo kupitia kinywaji cha Mo Xtra wakiwa na imani utawasaidia na kuendeleza walipoishia mwaka jana.

**"Udhamini wa mwaka jana tumeona faida yake, Simba ilifika hatua ya robo fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa na kutetea taji lao la ubingwa," alisema.**

Kwa upande wake Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Crescentius Magori, alisema ujio wa A One ndani ya klabu hiyo ni mafanikio makubwa ambayo anaamini yatasaidia kuzidi kutetea ubingwa wao msimu ujao unaotarajiwa kuanza kutimua vumbi mwezi ujao pamoja na kufanya usajili mzuri.

"A One kwetu tunaona ni mafanikio makubwa na neema ambazo zinazidi kuja kwetu, tumeishukuru kuamua kuendeleza ushirikiano na sisi kwa ajili ya kuendeleza timu yetu ,"alisema Magori.

Magori alisema kuwa msimu ujao wamepanga kufanya vizuri zaidi na kudai wanaendelea kufanya usajili ili kujiimarisha kwa ajili ya Ligi Kuu na michuano ya kimataifa.



Beki wa Timu ya Taifa ya Uganda, Hassan Wasswa, akimiliki mpira dhidi ya kiungo wa Misri, Mohamed Elneny, kwenye mechi ya Kundi A ya Fainali za Afcon iliyopigwa juzi nchini Misri na wenyeji kushinda kwa mabao 2-0.
**PICHA: MTANDAO**

# *Kocha Nigeria akiri Madagascar si ngoma ya kitoto*

**Na Somoe Ng'itu,** CAIRO

KATIKA hali isiyotarajiwa, Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Nigeria (Super Eagles), Gernot Rohr, amesema kuwa kikosi chake hakijashangazwa na kipigo ambacho walikipata kutoka kwa Madagascar, kutokana na kiwango kilichoonyeshwa na timu hiyo kwenye fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon) 2019, zinazoendelea nchini Misri.

Super Eagles juzi usiku ilikubali kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Madagascar na kuwafanya wamalize katika nafasi ya pili kwenye Kundi D wakiwa na pointi sita, Madagascar ambao wana pointi saba ndio vinara wa kundi hilo.

Akizungumza baada ya mchezo huo juzi usiku, Rohr, alisema kuwa Madagascar ina wachezaji wazuri na wanaocheza kwa nidhamu wakati wote wa mchezo.

Rohr alisema anaipa nafasi timu hiyo inayoshiriki fainali hizi kwa mara ya kwanza kufika mbali kwenye michuano hii inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf).

"Wana timu nzuri, wana timu bora, hata ukiangalia katika safari ya kufuzu kucheza fainali hizi, wao ndio walikuwa wa kwanza kukata tiketi, hatujisikii aibu kufungwa na kikosi cha aina hii," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa sababu nyingine ya kikosi chake kupoteza mchezo huo ilikuwa ni mabadiliko ya wachezaji watano wapya aliowatumia na hii ilitokana na tayari kuingia katika mechi hiyo wakiwa wameshafuzu hatua inayofuata.

"Tuliingia uwanjani tukiwa hatuna presha yoyote, kwa sababu tayari tulifuzu kucheza hatua ya 16-bora, niliamua kupumzisha baadhi ya wachezaji wangu wa kikosi cha kwanza, pia kutoa nafasi kwa wengine kuonyesha uwezo wao, hili ni shindano kubwa na kila mchezaji hufurahi anapopata nafasi ya kulitumikia taifa lake," alisema Rohr.

Mfaransa Nicolas Dupuis anayeiongoza Madagascar, alisema kuwa walijiandaa kuja kushindana katika fainali hizi na hicho ndicho wanachokifanya.

"Tumecheza na timu ngumu, kuifunga Nigeria haikuwa kazi nyepesi, Burundi pia walikuwa wazuri, tunazidi kuamini tutafanya vizuri mechi zinazofuata," Dupuis alisema.

Michezo

Jumanne Julai 2, 2019

Nipashe



Asensio sasa chambo ya Mane kutua Real UKURASA 30

# Samatta akataa kumfuata Origi

## ●●● Nyota huyo wa Liverpool sasa naye akunwa kuitumikia Harambee Stars, awapigia simu na kueleza...

**Na Somoe Ng'itu,** CAIRO

WAKATI ushindi wa mabao 3-2 ambao timu ya Taifa ya Kenya (Harambee Stars) iliupata dhidi ya Tanzania (Taifa Stars) ukirejesha "mapenzi" ya nchi zao kwa baadhi ya wachezaji wa Afrika Mashariki wanaocheza soka Ulaya, nahodha wa Stars, Mbwana Samatta ameapa kutoikana nchi yake kama ilivyo kwa Divock Origi, imeelezwa.

**Rais wa Shirikisho la Soka la Kenya (KFF), Nicky Mwendwa na Makamu wake, Doris Petra, wameliambia gazeti hili kwamba wamepokea salamu kutoka kwa mshambuliaji wa Liverpool, Divock Origi, kuwa anatamani kuwa mmoja wa nyota wa Harambee Stars.**

Origi ambaye aliisaidia Liverpool kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliomalizika, ana uraia wa Ubelgiji na anaichezea timu ya taifa ya nchi hiyo.

Petra alisema salamu hizi zimewafanya wajisikie faraja na nyota huyo amekuwa akizungumza na wachezaji wenzake kuwapa hamasa ya kuendelea kujituma.

"Tumefanya vema, tumefika katika hatua nzuri, angalia kijana kama Origi ambaye yeye na baba yake walikuwa hawataki kuisikia Kenya, sasa wanaitamani, ni hatua kubwa, ninaamini tutafanya vizuri zaidi," alisema Petra.

Aliongeza kuwa ushirikiano ambao wameupata kutoka kwa serikali, wachezaji wa zamani na wadau wa soka wa Kenya, ndio umewafikisha hapo na sasa Harambee Stars imekuwa ikipewa heshima yake inayostahili.

"Hata tulipofungwa na Algeria, hatukuachana, tulikuwa pamoja, nguvu hiyo ilitupa ushindi na ilitufanya pia tuifunge Tanzania, ari ilikuwa juu, tunamshukuru Mungu, kumbuka tulicheza Afcon ya mwisho mwaka 2004," aliongeza kiongozi huyo.

Origi aliyezaliwa mwaka 1995, ni mtoto wa mchezaji mkongwe wa Kenya, Mike Origi na alianza kucheza soka lake katika klabu ya Lille ya Ufaransa.

Lakini wakati Origi akitamani kurejea Harambee Stars, Samatta, ambaye naye anacheza soka la kulipwa nchini Ubelgiji akiitumikia Klabu ya KRC Genk amesema kikosi cha timu hiyo kimepanda "daraja" baada ya kushiriki fainali za Afcon 2019, na amefunguka kwamba hafikirii na hana mawazo ya kubadili uraia wa nchi yake ya kuzaliwa.

Samatta amekuwa nahodha wa kwanza wa kizazi hiki kuiongoza Taifa Stars kushiriki fainali hizo, baada ya Mwenyekiti wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na Rais wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Leodegar Tenga kukiongoza kikosi hicho katika fainali zilizofanyika Lagos, Nigeria mwaka 1980.

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalumu, Samatta alisema anajivunia kuwa Mtanzania na hatakubali kushawishika kuukana uraia wake kama baadhi ya wachezaji wa Afrika wanaong'ara barani Ulaya, ambao wamewahi kufanya hivyo.

Samatta alisema kuwa anaamini safari ya mafanikio ya Stars imeshaanza na watahakikisha wanasonga mbele kwa kuhakikisha wanapata tena nafasi kushiriki mashindano mengine yajayo na kufanya vema katika michuano mingine.

"Sheria za Ubelgiji ukiishi pale miaka mitano wanakupa hati yao ya kusafiria, lakini ni uamuzi wao sasa na akili yako, kinachofuata," alieleza nyota huyo ambaye pia ni balozi wa Utalii Tanzania.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa African Lyon (Mbagala Market) na Simba za jijini Dar es Salaam alisema kwamba kila mchezaji wa Tanzania sasa ana kiu ya kucheza soka la kulipwa na hali hiyo itasaidia kuwajenga na hatimaye kuwa na Stars yenye kiwango cha juu.

Stars jana usiku ilicheza mechi yake ya mwisho ya hatua ya makundi dhidi ya Algeria ikiwa ni baada ya kupoteza mechi zake mbili dhidi ya Senegal kwa mabao 2-0 na dhidi ya Harambee Stars 3-2.



Mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Misri, Mohammed Salah, akipiga hesabu ya kumtoka beki wa Uganda, Godfrey Walusimbi kwenye mechi ya Kundi A ya michuano ya Afcon iliyopigwa juzi nchini Misri na wenyeji kushinda 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga yataja kikosi kazi

**Na Faustine Feliciane**

KLABU ya Yanga chini ya Mwenyekiti wake, Mshindo Msolla, imezidi kujipanga baada ya jana kutangaza Kamati mpya ya Fedha na Mipango inayoundwa na watu 10 ikiwa chini ya Mwenyekiti, Arafat Haji akisaidiwa na Shija Richard, ambaye atakuwa makamu mwenyekiti.

Aidha, Deo Mutta ameteuliwa kuwa katibu wa kamati hiyo ambayo kwa mujibu wa Msolla itakuwa na wajumbe saba katika kuhakikisha wanafikia malengo ya kuisaidia klabu hiyo.

Wajumbe saba wanaoungana na viongozi hao kuunda kamati hiyo ni nahodha wa zamani wa Klabu ya Yanga, Ally Mayay, Said Kambi, Pindu Luhoyo, Baraka Katemba, Suma Mwaitenda, Haruna Batenga pamoja na Ivan Tarimo.

Alisema kamati hiyo itakuwa na kazi ya kusaidia uongozi kufikia malengo yao katika ukusanyaji wa fedha na mipango.

Msolla alisema hiyo ni kamati ya kwanza kuundwa na uongozi mpya ulioingia madarakani hivi karibuni kufuatia uchaguzi uliofanyika jijini Dar es Salaam Mei mwaka huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002